SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**RC** asisitiza wananchi kuchanja UVIKO- 19

UKURASA 9




**DYBALA APONDA SOKA LA JUVENTUS**

UKURASA 22


# Nipashe

Jumatatu Januari 17, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580828

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper


# NI JANGA

●●● **Moto** wateketeza Soko la Mchikichini, timu yaundwa kuchunguza, Samia, Mpango watuma salamu... *Endelea ukurasa 2*



Baadhi ya wafanyabiashara waliounguliwa bidhaa zao katika Soko la Ilala Mchikichini jijini Dar es Salaam wakiangalia masalia ya mali zao zilizoteketezwa kwa moto uliozuka usiku, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Wakulima wagoma kuuza korosho

UKURASA 3

## Wiki ya mchujo U-spika

UKURASA 4

**MICHEZO** **SIMBA WAPANIA 3 ZA MBEYA CITY LEO** UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Waziri Mkuu mstaafu Samwel Malecela, alipomtembelea kumjulia hali nyumbani kwake Kilimani mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Ni janga, moto wateketeza Soko Mchikichini

**Na Elizabeth Zaya**

VILIO na simanzi vilitawala jana kutoka kwa wafanyabiashara wa Soko la Karume Mchikichini, Ilala jijini Dar es Salaam, baada mali zao kuteketezwa kwa moto uliozuka, saa tisa usiku wa kuamkia jana.

Baadhi ya wafanyabiashara baada ya kufika katika eneo la tukio na kushuhudia mali zao zikiteketea, waliangua vilio, huku Jeshi la Polisi, Jeshi la Zimamoto na Kikosi cha Msalaba Mwekundu (REDCROS) vikifanya kazi ya kuimarisha ulinzi na kuwasaidia baadhi yao walionekana kuishiwa nguvu.

Nipashe lilishuhudia, baadhi ya wafanyabiashara wakiangua vilio, wengine wakiwa wamekaa chini huku wakiwa hawaamini kilichotokea.

Jeshi la Polisi lilionekana likitumia nguvu kumzuia mama mmoja aliyekuwa na mtoto mgongoni akitaka kuingia katikati ya moto kama mtu aliyechanganyikiwa.

“Niacheni niingie ndani, inauma sana, hapa ndipo nategemea kuendesha familia yangu, sasa itakuwaje, serikali inasema inatoa elimu bure, lakini hiyo elimu bure haina maana kama na mimi sijapambana kuja hapa kutafuta pesa ili watoto wangu wale,” alisikika mama huyo akizungumza hayo huku askari polisi wakimzuia asiingie katikati ya moto huo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wafanyabiashara wa soko hilo, walisema hakuna chochote walichookoa na hawaelewi wataendeshaje maisha yao kwa sasa.

Sharima Meshaki, alisema baadhi yao wamekopa pesa benki na hawaelewi watalipaje madeni yao hayo.

Masudi Issa, msemaji wa wafanyabiashara wadogo Mkoa wa Dar es Salaam, aliwataka wafanyabiashara wote katika soko hilo kuwa na subira wakati serikali inafanya tathmini na kuja na jibu.

“Serikali imekuja hapa na imechukua mawazo yetu ya namna gani ya kutusaidia ikiwamo kutengeneza soko jingine, kwa hiyo katika kipindi hiki tuvumilie, inaumiza kwa sababu mali zimepotea, lakini tuwe na subira,” alisema Issa.

**RED CROSS YASAIDIA**

Mshauri Idara ya Habari na Maafa wa Shirika la Msalaba Mwekundu (Red cross), Ombeni Kaizer, alisema katika tukio hilo, watu tisa waliathirika na wengine sita kuonekana kuchomwa na vitu vyenye ncha kali na kuwapatia huduma ya dharura ikiwamo ushauri wa kisaikolojia kutokana na mshtuko baada ya mali zao kuungua.

“Mpaka sasa, tumewasaidia watu tisa ikiwamo kuwapatia msaada wa kisaikolojia ambao walionekana kuathirika sana kutokana na mshtuko baada ya vitu vyao kuungua, kati ya hao sita walionekana kuchomwa pia na vitu vyenye ncha kali kama misumari,” alisema Kaizer.

“Kati ya hao tisa, pia kuna mama ambaye alitaka kupenya kwenye moto akiwa amebeba mtoto mgongoni, alichanganyikiwa, lakini tulimzuia na kumpatia ushauri na sasa anaendelea vizuri.”

**DC AUNDA TIMU**

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng’wilabuzu Ludigija, alisema wameunda timu ya uchunguzi wa tukio hilo ambayo itafanya kazi kwa siku 14 kutoa majibu ya chanzo cha moto huo pamoja na hasara yake.

Alisema timu hiyo itajumuisha, ofisi yake, ofisi ya Mkurugenzi, Jeshi la Polisi, Kikosi cha Uokoaji na TANESCO.

Hata hivyo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, baada ya kusikia malalamiko ya wafanyabiashara amepunguza siku za uchunguzi kutoka 14 hadi saba.

Alitoa agizo kwa wakuu wa mikoa wote nchini kutumia ripoti itakayotolewa na timu hiyo kudhibiti majanga ya moto katika masoko mbalimbali kwenye mikoa yao.

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Ashatu Kijaji, amesema wizara itashirikiana na TAMISEMI kuhakikisha wafanyabiashara wanarudi katika hali zao za kawaida.

“Taarifa ya moto tuliipata saa tisa kwenda saa kumi alfajiri, lakini mpaka sasa chanzo chake hatujajua japokuwa tunaambiwa unaweza kuwa umeanzia kwenye eneo la mama lishe, taarifa nyingine ni kwamba baadhi ya wafanyabiashara walikuwa wanajiunganishia umeme kinyemela. Lakini haya yote hatuwezi kusema ndiyo chanzo, baada ya timu ya uchunguzi ambayo nimeiteua ambayo itaanza kazi kesho (leo) ndiyo itatupatia majibu ya haya yote,” alisema Ludigija.

“Baada ya uchunguzi huo, ndio tutasema chanzo hasa ni nini. Na kwa sababu karibu mali zote na vitu vyote vilivyokuwa kwenye soko hili vimeungua kwa zaidi ya asilimia 98, ndiyo maana tunasema mali zote zimeungua.”

Alisema tathmini halisi ya chanzo na mali zilizoungua itatolewa baada ya timu hiyo kumaliza kazi yake ndani ya wiki mbili kuanzia leo.

Alitoa wito kwa wananchi na wafanyabiashara kujiepusha na maneno yoyote ya upotoshaji kuhusu tukio hilo na kuwataka kuwa watulivu katika kipindi ambacho uchunguzi huo unafanyika.

Alisema Jeshi la Polisi litaendelea kuimarisha ulinzi na kufanya doria wakati wote mpaka taarifa ya uchunguzi itakapokamilika.

Pia alisema kutokana na tukio hilo, Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, wametuma salamu za pole kwa wafanyabiashara hao na kuwataka kuwa watulivu.

“Rais wetu Samia Suluhu Hassan na Makamu wa Rais Dk. Mpango, wametoa salamu za pole kwa wafanyabiashara ambao wamepoteza mali zao kutokana na moto huu, wameniambia niwape pole sana wafanyabiashara kwa tukio hili,” alisema Ludigija.

“Wamesema katika kipindi hiki ambacho moto umetokea, tuwaombe wafanyabiashara na wananchi wanaozunguka maeneo haya, wawe watulivu wakati tunaenda kufanya uchunguzi.”

**WASEMA SIKU 14 NYINGI**

Baadhi ya wafanyabiashara, wamesema siku 14 zilizotolewa kwa ajili ya uchunguzi ni nyingi na kwamba ni vyema wangeruhusiwa kujenga vibanda vya muda wakati wanasubiri ripoti kamili ili waendelee kufanya biashara na kusaidia familia zao.

“Tuliamini kwamba mheshimiwa alivyokuja hapa angetupa pole, halafu angesema baada ya zimamoto kumaliza kazi yake, aturuhusu kujenga mara moja vibanda ili tuendelee na kazi, hatukubaliani na huo muda waliouweka kwa sababu ni mrefu sana, tutaishije,” alilalamika Mariam Muya, mmoja wa wafanyabiashara katika eneo hilo.

“Sisi hatuwezi kuishi bila Karume, watoto wangu wote wanaishi kwa kutegemea hapa, tunaomba waturuhusu tujenge vibanda, hatuondoki hapa na hatuko tayari kusubiri hizo siku zote hata kama watatupiga mabomu.”

Hadija Ramadhani, mfanyabiashara katika eneo hilo, alisema mara ya kwanza soko hilo lilipoungua waliambiwa hivyo, lakini hawakusaidiwa, hivyo ni vyema waruhusiwe wajenge wenyewe na waanze kufanya biashara.

Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Masauni naye ametuma salamu za pole kwa wafanyabiashara hao na kuwaomba kuwa watulivu katika kipindi ambacho vyombo vya ulinzi na usalama vinafanya uchunguzi kubaini chanzo cha moto huo.

Aliliagiza Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini chanzo kwa kushirikiana na wataalamu na kamati iliyoundwa na serikali kuchunguza tukio hilo ili matukio hayo yasijirudie tena.

Alilipongeza kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama, kufanikiwa kudhibiti moto huo kutoleta madhara zaidi katika maeneo ya jirani.


**TANGAZO!!**
**AFRIWELD INDUSTRIES LTD**
**Nafasi ya kazi**

Wanahitajika wasichana Wenye umri kuanzia miaka 25-35
**Nafasi:** Mauzo
MSHAHARA wa kuvutia utatolewa!! wahi sasa Kupata nafasi nzuri!!
Kwa mwasiliano zaidi piga simu namba: **0719 184 070**
Piga simu muda wa kazi TU saa MBILI mpaka saa KUMI NA MOJA jioni
01/01/2022 MPAKA 31/01/2022
**Asante**
116653602



**KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI**

**WINFRIDA ALBOGAST MOSHA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC 709 CLN.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **IRI/IRI/RB/18671/2022.**
116653402

HABARI KITAIFA

# UDSM yampa tuzo Rais Samia



**Na Beatrice Shayo**

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka (pichani), amemtaja Rais Samia Suluhu Hassan, kuwa turufu ya maendeleo ya Watanzania kutokana na falsafa tatu anazotumia katika uongozi wake ambazo ni upangaji, usimamiaji na utekelezaji.

Aidha, amemtaja Mkuu huyo wa nchi ambaye ni Mwenyekiti wa CCM, kuwa ni mwanadiplomasia nguli wa uchumi na hilo linadhihirika kwa namna alivyopata mkopo nafuu kutoka Shirika na Fedha la Kimatafa (IMF) na namna alivyopanga matumizi yake.

Shaka aliyasema hayo jijini Dar es Salaam wakati akipokea tuzo ya kumpongeza Rais Samia kwa utendaji mzuri, iliyotolewa na Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM), Tawi la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Alisema Rais Samia amekuwa turufu ya maendeleo ya Watanzania kutokana na falsafa tatu anazozitumia katika uongozi wake ambazo ni upangaji, utekelezaji na usimamiaji.

Kwa mujibu wa Shaka, hayo yamejidhihirisha katika uongozi wake kwa kipindi cha miezi tisa kwa kutekeleza

Ilani ya Uchaguzi ya CCM mwaka 2020-2025, kwamba wanaamini kufikia mwaka 2025 utekelezaji utazidi asilimia 100.

"Kwa kipindi hiki kifupi cha uongozi wake, leo hii ukimsimamisha Mkuu wa Wilaya yeyote akueleze mafanikio, atatumia zaidi ya saa nane kueleza kazi kubwa ambayo imefanywa kwa muda mchache," alisema.

Alisema Rais Samia amekuwa kiongozi ambaye kila anachokikusanya anahakikisha kinakwenda katika shughuli lengwa, jambo linalothibitisha usimamizi mzuri. Alimtaja mkuu huyo wa nchi kuwa mwanadiplomasia nguli wa uchumi kutokana na kile alichoeleza kwamba, amefanikisha upatikanaji wa mkopo nafuu Sh. trilioni 1.3 kutoka IMF na ameuelekeza katika matumizi sahihi.

Alisema, fedha hizo zimeongeza mzunguko nchini na kufanya kipato cha kila Mtanzania kuongezeka.

Kuhusu tuzo hiyo waliyomkabidhi Rais Samia, alisema ni ishara ya vijana kuiunga mkono serikali ya awamu ya sita.

Aliwataka vijana kuwa mabalozi wazuri wa Rais Samia kwa kueleza mazuri anayofanya, akiwasihi wasipofanya hivyo hakuna mtu wa nje ya nchi atatekeleza hilo badala yao.

"Mcheza kwao hutunzwa basi nanyi vijana hakikisheni mnakuwa mabalozi wazuri wa Rais wetu, ni sisi ndiyo wa kumtia moyo hakuna mwingine atakayefanya hivyo badala yetu," alisema.

Aliahidi kuandaa darasa la itikadi kwa ajili ya kuwaelimisha vijana, wafahamu nchi ilipotoka, ilipo sasa na inapoelekea.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa UVCCM Tawi la UDSM, Isack Sambuli, alisema tuzo hiyo waliyotoa kwa Rais Samia imetokana na utendaji mzuri aliouonyesha kwa kipindi kifupi.

Aliahidi kumtetea na kumuunga mkono wakati wote, akisema vijana hawatarudi nyuma katika hilo.

# Ajali ya treni yaua, yajeruhi watano

**Na Christina Mwakangale**

SHIRIKA la Reli Tanzania (TRC), limesema ajali ya treni iliyotokea eneo la Mkalamo-Mvave, imesababisha kifo cha mtoto Hassan Lugano na kujeruhi watano.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa umma na Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa Shirika hilo, Jamila Mbarouk, chanzo cha ajali hiyo ni mabehewa matano kupinduka na mengine manne kuacha njia.

"Shirika la Reli Tanzania, linautaarifu umma kuwa treni ya abiria yenye injini namba 9022 imepata ajali majira ya saa 10 alfajiri kati ya Mkalamo na Mvave, Wilaya ya Pangani mkoani Tanga, Januari 16.

"Treni hiyo iliondoka Arusha, saa 8:30 mchana siku ya Jumamosi, kuelekea Dar es Salaam ikiwa na behewa 14 zilizobeba abiria 700, ilipofika eneo lililoko kati ya Mkalamo na Mvave (km 88) behewa tano zilipinduka na kusababisha majeruhi watano, wanaume watatu, wanawake wawili na kifo cha mtoto," alisema Jamila kwenye taarifa hiyo.

Kadhalika, alitaja behewa hizo zilizopinduka kuwa ni namba 3614, 3527, 3605, 3526 na 3530 na zilizoacha njia ni zenye nambari 3662, 3666, 4536 pamoja na behewa la huduma ya chakula na vinywaji 'buffet'. "Majeruhi wamepelekwa katika zahanati ya Mkalamo kwa ajili ya kupatiwa matibabu na wanaendelea vizuri, shirika linaendelea na taratibu nyingine kurejesha huduma za usafiri," alisema Jamila.

Pia alisema shirika linaendelea kufuatilia kwa karibu chanzo cha ajali ili kuchukua hatua, huku likitoa pole kwa familia ya marehemu na kuwaombea majeruhi wa ajali kupata nafuu mapema na kuendelea na majukumu yao ya kujenga taifa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Safia Jongo, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo akisema kifo ni kimoja cha mtoto pamoja na majeruhi watano ambao hali zao zinaendelea vizuri na kupatiwa matibabu. "Ajali imetokea Mkoa wa Tanga wilayani Handeni, katika mabehewa matano katika ajali hiyo kuna kifo cha mtoto, majeruhi watano na waliojeruhiwa wanaendelea na matibabu, pia abiria waliokatiza safari shirika linawashughulikia ili kuendelea na safari," alisema Kamanda Jongo.

# Wakulima wagoma kuuza korosho kwa bei ndogo

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

WAKULIMA wa korosho wilayani Tunduru, mkoani Ruvuma, wamegoma kuuza korosho zao baada ya kutokea kasoro kadhaa ikiwamo bei ndogo iliyotolewa na wanunuzi waliojitokeza katika mnada wa 12 uliofanyika katika ghala la Chama cha Msingi Mlingoti Magharibi (AMCOS).

Kutokana na dosari hizo mwakilishi wa Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Wilaya ya Tunduru (TAMCU), Pino Chipojola, alilazimika kuahirisha mnada huo hadi wiki ijayo.

Akizungumzia kasoro hizo, Chipojola alisema wanunuzi waliojitokeza waliomba kununua korosho kutoka katika ghala moja kati ya maghala makuu matatu ya mnada yanayopokea korosho kutoka kwenye maghala madogo ya vyama vya msingi AMCOS.

Kwa mujibu wa Chipojola, kasoro ya pili ilikuwa ni wanunuzi kutoa bei ndogo ambayo haiendani na gharama walizotumia wakulima wakati wa uzalishaji wa zao hilo ambazo bei ya chini ilikuwa Sh. 1,400 na ya juu Sh. 1,650.

Awali, Ofisa Ushirika wa Wilaya ya Tunduru, George Bisani, alisema jumla ya tani za korosho 347,547 na wanunuzi wanne waliomba kuzinunua kwa wastani wa Sh. 1,450 fedha ambayo baada ya makato ya tozo zote mkulima angepata Sh. 1,150 ambayo haiendani na gharama walizozitumia wakati wa uzalishaji.

Aidha, Bisani aliwapongeza wakulima hao kwa uamuzi waliouchukua kuwa umesaidia kuondoa mgogoro ambao ungeweza kujitokeza kwa wakulima ambao korosho zao zisingeuzwa pamoja na watunza maghala ambao korosho zao zisingeuzwa.

Mwakilishi wa Meneja wa Bodi ya Korosho tawi la Tunduru, Enock Ngalaba, alishangazwa na utaratibu uliotumiwa na wanunuzi hao wakidai kuwa korosho za maghala yote zilitumwa mtandaoni zikiwa na ubora unaofanana.

Kuhusu malalamiko ya bei zinazolalamikiwa na wakulima katika msimu huu, alikiri kuwapo kwa ujanja kutoka kwa wanunuzi ambao wamekuwa wakitoa bei ndogo kwa kusingizio cha ugonjwa wa UVIKO-19 kuwa ndiyo ulioathiri soko la mazao.

Kutokana na hiyo, Ngalaba aliwaomba wanunuzi kuboresha bei wanazotoa ili kumsaidia mkulima na kumwezesha kupiga hatua za kimaendeleo kulingana na jasho lake.

Wakiongea kwa nyakati tofauti, baadhi ya wakulima walioshiriki katika mnada huo waliiomba serikali kudhibiti vitendo hivyo vinavyoonekana kutaka kuhujumu mfumo huo.


FSSP Field Support Services Project | Tanzania

## CONSULTANCY POSITION FOR PROFESSIONAL RAPPORTEUR AND TRANSLATION EXPERTS

PricewaterhouseCoopers Limited (PwC) invites eligible candidates to indicate their interest to provide individual consultancy services as Professional Rapporteur & Translator to the Field Support Services Project (FSSP) Tanzania. .

The experts will provide technical support and advice to Global Affairs Canada and its implementing partners.

A candidate is eligible to apply for one or both two positions. The minimum key qualifications for each position are as outlined below..

1. **Rapporteur services:**
   - A bachelor's degree in Secretarial services, Languages or other social studies, from a recognized institution.
   - Skills in short handwriting, preferably with a speed of 200 words per minute.
   - Typing skills, preferably with a speed of 60 words per minute.
   - 5 years' Work experience in providing rapporteur services to or for international development programmes. At a minimum candidate should have experience leading the development, writing, and drafting/editing of technical reports or proceedings.
2. **Translation services**
   - A bachelor's degree in Languages or other social studies, from a recognized institution.
   - 5 years' Work experience in providing translation and interpretation services (English – Swahili and vice versa).
   - Demonstrated experience in translation of professional/official documents (English – Swahili and vice versa) for international development programmes.
   - Proven experience of working with international development organizations/agencies.
   - Proven experience in providing transcription services

In addition to the key qualifications above, the incumbent is also expected to demonstrate the skills and competencies in Advanced professional proficiency in spoken and written English – level 4 and Kiswahili – level 4 as explained in **http://www.international.gc.ca/ifait-iaeci/test_levels-niveaux.aspx?lang=eng**

Interested individual candidates may obtain detailed description of these services by sending a request email to **procurement@fssptz.org.** Requests for further information will be received up to three working days prior to the submission deadline. Any request received later than that may not be responded to.

Interested candidates should send their Expressions of Interest (EoIs) ONLY electronically to **procurement@fssptz.org** not later than **26th January 2022 at 23:59 hours.** Late Expressions of Interest shall not be accepted for evaluation, irrespective of the circumstances.

166503

# Ni wiki ya mchujo U-spika wa bunge

**Na Mwandishi Wetu**

NI wiki ngumu kwa makada 71 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), waliojitokeza kuchukua fomu za kuomba kuteuliwa kuwania nafasi ya Spika wa Bunge.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa Januari 9, mwaka huu, na Katibu Idara ya Itikadi na Uenezi wa chama hicho, Shaka Hamdu Shaka, urejeshaji fomu ulikamilika Januari 15.

Makada hao wa CCM wamejitokeza kuwaniwa kiti hicho, baada ya Spika wa Bunge, Job Ndugai, kujiuzulu wadhifa huo, Januari 6, mwaka huu.

Leo Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama hicho itakutana kwa ajili ya kujadili wagombea na kuishauri Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) wagombea waliojitokeza kuomba kiti hicho.

Januari 18 na 19, itakuwa ni kazi ya kuchuja na kufanya uteuzi wa mwisho utakaofanywa na Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu.

Kabla ya kupigiwa kura na wabunge wote, Janauri 21 hadi 30 itakuwa ni kikao cha chama cha wabunge wa CCM (caucus), kupiga kura kumpata mgombea ambaye atakwenda kuomba kura bungeni.

Miongoni mwa waliojitokeza kwenye kinyang'anyiro hicho ni Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, aliyewahi kuwa Mwenyekiti wa UWT Taifa, Sophia Simba na aliyewahi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mbunge wa Jimbo la Bariadi (CCM), Andrew Chenge.

Vile vile, kiti hicho kinawaniwa na wabunge mbalimbali akiwamo Joseph Kasheku, maarufu Msukuma, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais Bunge la Afrika (PAP) na Mbunge wa Shinyanga Mjini, Steven Masele na msomi aliyejinasibu kuwa na shahada tisa, Baraka Byabato.

Hadi juzi watu 71 walikuwa wamejitokeza kuchukua fomu za kuwania nafasi hiyo, ambayo ilitolewa kwa gharama ya shilingi milioni moja.

Kuanzia leo itakuwa wiki ya mchakato wa kumpata kada atakayekiwakilisha chama hicho kwenye kinyang'anyiro cha kumpata Spika mpya wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kifungu cha 84.-(1) kutakuwa na Spika wa Bunge ambaye atachaguliwa na wabunge kutoka miongoni mwa watu ambao ni wabunge au wenye sifa za kuwa wabunge; atakuwa ndiye kiongozi wa Bunge na atawakilisha Bunge katika vyombo na vikao vingine vyote nje ya Bunge.

TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

TAARIFA KWA WASAFIRISHAJI

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inawakumbusha Wafanyabiashara wote wa usafirishaji kufika kwenye ofisi zetu au kupitia mifumo yetu kwa ajili ya kulipa kodi ya mapato awamu ya kwanza.

*Epuka usumbufu na adhabu kwa kutokuwa na stika ya mapato!.*

Imetolewa na;

MKURUGENZI HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI

*"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"*

# Njombe yapewa mabilioni miradi maendeleo

**Na Jenifer Gilla**

MSEMAJI Mkuu wa Serikali, Greyson Msigwa, amesema kwa kipindi cha miezi tisa serikali imetoa Sh. bilioni 375.4 zilizoelekezwa kwenye miradi ya maendeleo mkoani Njombe.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani humo kuhusu kazi iliyofanywa na serikali kwa kipindi cha miezi tisa tangu Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani, alisema Sh. bilioni 277 zimeelekezwa kuboresha miundombinu ya barabara ili kuongeza tija kwenye kilimo.

"Kwa kuwa Njombe ni mkoa wa kilimo, na kwa sehemu kubwa kilimo kinategemea miundombinu ya barabara, ndiyo maana sehemu kubwa ya fedha hizi tumeelekeza huko kupitia Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA)," alifafanua Msigwa.

Aidha, alisema Sh. bilioni 7.2 zimeelezwa sekta ya afya kupitia mpango wa taifa wa mapambano dhidi ya UVIKO-19 imetoa Sh. bilioni 4.7.

Vile vile, imepeleka katika mkoa huo Sh. milioni 150 kutoka kwenye tozo za miamala ya simu ambazo zimeelekezwa kwenye ujenzi wa madarasa, Sh. bilioni 1.75 kwa ajili ya vituo vya afya na Sh. bilioni 24 zimetolewa kwa ajili ya kununulia dawa kupitia Bohari Kuu ya Dawa (MSD).

Alisema fedha nyingine Sh. bilioni 11 zimetolewa na Serikali Kuu ikiwa ni mgawo wa serikali kwa ajili ya ujenzi wa zahanati na vituo vya afya na nyingine zimetumika kujengea Hospitali ya Rufani Njombe.

Kwa mujibu wa Msigwa, miradi mingine inayoendelea mkoani humo inayotekelezwa kupitia fedha hizo kuwa ni ujenzi wa barabara ya Njombe-Makete yenye urefu wa kilometa 107.4, Njombe - Moronga yenye urefu wa kilomita 53.9 uliogharimu Sh. bilioni 109.2 ambao umekamilika kwa asilimia 95.68.

Aliitaja pia barabara ya Moronga - Makete yenye urefu wa kilomita 53.5 ambao ujenzi wake utagharimu Sh. bilioni 110 na ujenzi umefikia asilimia 86, pamoja na barabara ya Itoni-Bubelwa -Manda yenye urefu wa kilomita 211, kipande cha pili barabara ya Lusitu-Mawendi yenye urefu wa kilomita 50 kwa zege kitachogharimu Sh. bilioni 159 uliokamilika kwa asilimia 83.46.

Pia kipande cha barabara ya Itoni - Lusitu uliofikia asilimia 50 ambao taratibu za kumpata mkandarasi kuanza ujenzi zinaendelea.

**MRADI MAKAA YA MAWE**

Kuhusu mradi wa makaa ya mawe wa Liganga na Mchuchuma ulioko Wilaya ya Ludewa, Msigwa alisema kuwa serikali inatambua umuhimu wa mradi huo na inaufuatilia kwa karibu.

"Sasa hivi kuna majadiliano yanayoendelea kati ya serikali na mwekezaji ili tukamilishe na aanze kazi mara moja," alieleza.

Alisema katika fedha hizo Sh. bilioni 277 zimeelekezwa kwenye kuboresha miundombinu ya barabara ili kuongeza tija kwenye kilimo. Aliongeza kuwa serikali kupitia mpango wa taifa wa mapambano dhidi ya UVIKO-19 imetoa Sh. bilioni 4.7. Vile vile serikali imepeleka katika mkoa huo Sh. milioni 150 kutoka kwenye tozo za miamala ya simu ambazo zimeelekezwa kwenye ujenzi wa madarasa, Sh. bilioni 1.75 kwa ajili ya vituo vya afya na Sh. bilioni 24 zimetolewa kwa ajili ya kununulia dawa kupitia MSD.

Msigwa aliitaja miradi mingine inayoendelea mkoani humo inayotekelezwa kupitia fedha hizo kuwa ni ujenzi wa barabara ya Njombe-Makete yenye urefu wa kilometa 107.4, Njombe - Moronga yenye urefu wa kilomita 53.9 uliogharimu Sh. bilioni 109.2 ambao umekamilika kwa asilimia 95.68.

TANGAZO

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI MPYA ZA STEMPU ZA KODI ZA KIELEKTRONIKI (ETS)

**Dar es Salaam, 17 Januari, 2022:**

Kwa mujibu wa Kanuni ya 6(2) ya Kanuni za Stempu za Kodi za Kielektroniki za Mwaka 2018, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) anapenda kutangaza bei mpya ambazo mtengenezaji, mzalishaji na muagizaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa na ambazo zimeorodheshwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni za Stempu za Kodi za Kielektroniki za mwaka 2018 atanunua stempu kutoka kwa Muuzaji aliyeingia mkataba na TRA yaani kampuni ya M/s SICPA Tanzania Ltd **kwa bei kama ilivyo hapa chini**;

| Na | Aina ya Bidhaa | Chanzo | Bei kwa Stempu 1,000 |
|---|---|---|---|
| 1 | Pombe Kali | Zote | **TZS 42,214.37** |
| 2 | Mvivyo wa Zabibu | Zote | **TZS 42,214.37** |
|  | Mvinyo wa Matunda | Wenye matunda ya Ndani kwa Asilimia 75 au zaidi | **TZS 17,435.37** |
| 3 | Sigara | Zote | **TZS 42,214.37** |
|  | Bidhaa Nyingine za Tumbaku |  |  |
| 4 | Bia | Zinazozalishwa Nchini | **TZS 18,312.91** |
|  |  | Zinazoingizwa toka Nje | **TZS 23,093.20** |
| 5 | Juisi za Matunda na Mbogamboga | Zinazozalishwa Nchini (Kwa matunda ya Ndani | **TZS 8,082.62** |
|  |  | Zinazoingizwa toka Nje | **TZS 15,264.61** |
| 6 | Maji ya Chupa | Zote | **TZS 8,082.62** |
| 7 | Vinywaji Laini | Zilizochini ya Tarrif namba 2202.10.00 | **TZS 8,082.62** |
|  |  | Vinywaji vingine chini ya tariff namba 2202.91.00 and 2202.99.00 | **TZS 15,264.61** |
| 8 | Bidhaa za Filamu na Muziki (yaani, CD/VCDs/DVD/Kanda zilizorekodiwa) | All | **TZS 16,165.24** |

**Bei hizi mpya zitaanza kutumika kuanzia tarehe ya tangazo hili.**

Kwa msaada na maelezo zaidi, TRA inawahimiza wafanyabiashara na umma kwa ujumla kutembelea katika ofisi za TRA zilizopo karibu, au kwa kutembelea tovuti ya TRA **(www.tra.go.tz)** au Kituo cha Huduma kwa Mlipakodi kinachopatikana kwa namba za kupiga bure **"Toll free" 0800 750 075** au **0800 780 078** au barua pepe **huduma@tra.go.tz**

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na;
**KAMISHNA MKUU**
**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Waamuzi wasiishie kumulikwa Ligi Kuu, Championship nako ni tatizo*

**KUMEKUWA** na malalamiko mengi ya kuboronga kwa baadhi ya waamuzi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea nchini, labda ni kwa sababu ndiko kuna timu pendwa zenye mashabiki wengi wa Simba na Yanga ndiyo maana sehemu kubwa za wanaopiga kelele na kukemea kuboronga kwa marefa ni wale wale wa timu hizo. Pia inawezekana ni kwa sababu watu wengi wanapata nafasi ya kuziangalia mechi nyingi za Ligi Kuu kuliko za Championship.

Ukweli ni kwamba hata huko pia kuna matatizo kama haya kwenye Ligi Kuu, kwani baadhi ya timu zimekuwa 'zikinyongwa mchana kweupe', kwa sababu huko hakuna ushahidi wa mechi kuonyeshwa kwenye televisheni, hivyo ni kama machozi ya samaki tu, yanabaki majini.

Hata hivyo, kama ilivyo Ligi Kuu, pia kwenye Championship kuna timu zimewekeza hasa ukitazama namna ambavyo zimefanyika usajili wa hali ya juu msimu huu, ambapo tumeshuhudia wachezaji wengi wa kigeni baadhi wakiwa wameshawahi kucheza timu kubwa za hapa nchini kama Simba, Yanga na Azam FC.

Mbali na Nipashe kuwa makini katika kufuatilia Ligi ya Championship na kujionea aina ya maamuzi mabovu ambayo yamekuwa yakitolewa, lakini tayari baadhi ya timu zimekuwa zikilalamikana na uchezeshaji mbaya kutoka kwa baadhi ya waamuzi, ingawa ni vigumu kwa mashabiki wengi kupaza sauti kutokana na kuwa 'bize' na klabu zao pendwa Simba, Yanga na Azam FC.

Lakini ikumbukwe kuwa ligi hiyo ndiyo inayotoa timu zinazopanda daraja kwenda kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara, hivyo uwapo wa waamuzi wanaongozwa na sheria 17 za soka na kutenda haki, ni muhimu ili timu zitakazopanda, ziwe zimestahili kweli na hatimaye kutoa ushindani mkubwa msimu ujao.

Tumeona kwa miaka ya hivi karibuni, timu zinazopanda Ligi Kuu kutoka chini, basi moja au mbili ni lazima zishuke tena daraja msimu huo huo, jambo ambalo linaonyesha kuwa huenda zilipanda kwa mbeleko za waamuzi, hivyo kushindwa kukabiliana na ushindani uliopo Ligi Kuu.

Kwani ni wazi kwamba kama timu ilipanda kwa kuungaunga, hakuna namna lazima itarudi tu ilikotoka, jambo ambalo linazidi kurudisha nyuma ukuaji wa soka letu kila uchao.

Lengo letu ni kutaka kuona kupungua kwa timu Ligi Kuu na kubaki 16, kunaongeza ushindani ili kuifanya ligi yetu kukua na kuwa kivutio, lakini kwa mwenendo huu wa maamuzi mabovu, tutazidi kuona tukipiga hatua mbili mbele na tatu nyuma.

Hivyo, wakati huu ambao tayari mzunguko wa kwanza umemalizika kwenye Ligi ya Championship, tunalikumbusha Shirikisho la Soka nchini (TFF), Bodi ya Ligi (TPLB) na Chama cha Waamuzi Tanzania (FRAT) kuwa makini na waamuzi wenu wanaochezesha mechi hizo kwa kufinyanga sheria 17 za soka.

Ni wakati sasa wa kuanza kuzifuatilia mechi hizo ili kukabiliana na madudu ya baadhi ya waamuzi ambao wanakwenda kinyume cha kiapo cha marefa cha kutoa maamuzi ya haki uwanjani kwa kutimiza sheria 17 za soka.

Tunaamini kama haki ikitendeka, timu zitakazopanda Ligi Kuu, zitaenda kutoa ushindani wa kweli na si kuishia tu kuwa wasindikizaji kwa kucheza msimu mmoja na unaofuata kushuka daraja. Lakini, ikumbukwe waamuzi wana nafasi kubwa zaidi ya kuliweka soka letu katika viwango vya juu endapo watatenda haki, hivyo ni matarajio yetu kwa baadhi ambao wanahadaika na kutanguliza maslahi yao binafsi, wataacha tabia hiyo mara moja.

Hivyo, TFF, TPLB na FRAT jicho la ziada linahitajika Ligi ya Championship ikiwa ni pamoja na kuwachukulia adhabu kali waamuzi wote watakaobainika kufinyanga haki kwa kutotekeleza sheria 17 za soka dimbani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# *TPLB msiogope lawama kufungia viwanja vibovu*

Na Adam Fungamwango

**UWANJA** wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani umefungiwa na Bodi ya Ligi nchini (TPLB), kutumika kwenye mechi za Ligi Kuu hadi hapo utakapofanyiwa marekebisho kwenye sehemu ya kuchezea 'pitch'.

Taarifa hiyo ilitolewa juzi na Idara ya Habari na Mawasiliano ya Bodi ya Ligi, ikisema tatizo kubwa linalotakiwa lifanyiwe kazi ni uwanja huo kusawazishwa vizuri na majani yake kustawishwa vema ili kuendana na matakwa ya kanuni na sheria namba moja ya soka inayozungumzia uwanja hususan eneo la kuchezea.

Ikumbukwe kuwa uwanja huo hutumiwa na timu ya Ruvu Shooting kama dimba lake la nyumbani.

Kwa maana hiyo, Bodi ya Ligi imesema kuwa timu hiyo sasa italazimika kuutumia Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam kama wa nyumbani hadi hapo ule wa Mabatini utakaporekebishwa.

Hivi karibuni TPLB iliufungia Uwanja wa Manungu Complex, uliopo Turiani mkoani Morogoro kutokana na kutokidhi matakwa kama hayo.

Na hii ilikuwa ni wiki chache tu baada ya kuufungulia. Kabla ya hapo uwanja huo ulikuwa umefungiwa na kutotumika kwa kiasi cha misimu miwili kutokana na kutokidhi matakwa ya kuuzungushia ukuta.

Pamoja na kwamba tayari umeshazungushiwa ukuta, bado haujamalizika vizuri, lakini kuna matatizo kwenye sehemu ya kuchezea, picha za televisheni wakati timu inayotumia uwanja huo Mtibwa Sugar ilipokuwa inacheza mechi yake ya Ligi Kuu, ilionekana kuna sehemu hakuna nyasi, zingine zipo, kiasi cha kuchekesha hata watu waliokuwa wakitazama mechi hiyo, kwani ilionekana ni kama shamba lenye vitalu.

Kuna baadhi ya watu wamekuwa wakiilaumu Bodi ya Ligi kwa kudai ni kwa nini wanavifungia viwanja hivyo baada ya kuona ubovu kwenye televisheni? Wengine wanadai kwani huwa havikaguliwi mwanzo? Nani alivikagua? Na kwa nini kuna wakati vinaruhusiwa na baadaye TPLB hiyo hiyo inayoviruhusu inakuja kuvifungia?

Haya ndiyo maswali na malalamiko ya wadau wa soka kwenye mitandao ya kijamii na katika mijadala mbalimbali ya michezo mitaani, redioni na kwenye televisheni.

Ukweli hapa ni kuwa, uwanja wa soka ni kama shamba, nyumba au binadamu. Ni leo inaweza kuwa hivi, lakini kesho ikawa vile. Binadamu anaweza kuamka leo mzima, kesho akawa mgonjwa.

Viwanja hivi awali huwa vinakaguliwa kabla ya kuanza ligi, na haiwezekani wakaguzi wakavikagua Agosti, basi vikabaki na ubora huo huo hadi Desemba au Januari. Hapa katikati vinatakiwa viendelee kutunzwa na wasimamizi wa viwanja.

Kuna ukame, matunzo mabovu na mvua kupita kiasi pia, vyote hivi vinasababisha ubovu wa uwanja. Na kama hatutokuwa na usimamizi mzuri uwanja hauwezi kuwa vile vile kama ulivyokaguliwa mwanzo. Na haiwezekani bodi iwe inasafirisha watu wake kukagua viwanja kila kabla ya mechi za Ligi Kuu kuchezwa.

Ndiyo maana unaona Bodi ya Ligi nayo wakati mwingine inatumia televisheni kuangalia uwanja uko kwenye hali ile ile kama ulivyokaguliwa na kama wakiona kuna tatizo wanaufungia.

Binafsi naipongeza Bodi ya Ligi kwa hatua inazochukua mara kwa mara kuvifungia kwa sababu lengo si kukomoana, ila ni kuviboresha kwa sababu vikiboreshwa havitakuwa vya TPLB bali vya wamiliki wenyewe.

Ndiyo maana tumeona kwa mara ya kwanza Uwanja wa Manungu Complex umezungushiwa ukuta na utabaki kuwa ni mali yao, lakini jitihada zimefanywa na Bodi ya Ligi ili uwe hivyo.

Na kwa bahati nzuri ni wepesi wa kufungulia viwanja mara vinapoonekana kukidhi vigezo wanavyovitaka.

Kwa hali yoyote hapa wa kulaumiwa kuhusu ubovu wa viwanja na kusababisha vifungiwe ni wamiliki wenyewe wa viwanja na si TPLB inayovikagua, kuvifungia na kuvifungulia. Wenyewe huwa wanavikagua, lakini baadaye vinaharibika kwa sababu mbalimbali, hilo sasa linakuwa si jukumu lao tena.

Na ni upotevu wa raslimali fedha kuanza kuvifuatilia kila uchao, wakati wamiliki wamekaa tu hawajali hadi wafungiwe.

HABARI KITAIFA




Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, akikagua ukuta unaotenganisha makazi ya watu na Bahari ya Hindi, Pangani jana. Kushoto ni Ofisa Mazingira wa Wilaya ya Pangani, Daud Mlahagwa, akitoa maelezo ya uharibifu wa mazingira katika ukuta huo, na Katibu Tawala wa wilaya hiyo, Mwalim Nyange (kulia). **PICHA: HANIDA KAMCHALA**

# Mwanafunzi mwenye ulemavu asaidiwa vifaa vya shule

**Na Said Hamdani,** LINDI

WAKATI shule za msingi na sekondari zikifunguliwa leo, uongozi wa Manispaa ya Lindi, umeahidi kumpatia vifaa vya masomo mwanafunzi mwenye mahitaji maalum, Hamisi Hassan Ahmadi (15) aliyefaulu kidato cha kwanza.

Mkurugenzi wa manispaa hiyo, Juma Nnwele, aliahidi hayo alipokuwa na mwanafunzi huyo, mzazi wake wa kike, Ofisa Maendeleo ya Jamii, Moses Mkoveke na waandishi wa habari, waliofika ofisini kwake kuangalia jinsi atakavvyosaidiwa vifaa vinavyohitajika.

Hamisi ni mwanafunzi mwenye ulemavu wa viungo na hulazimika kukaa kwa kutumia mgongo, aliyekuwa anasoma Shule ya Msingi Msinjahili, Manispaa ya Lindi na kupangiwa kuendelea na elimu ya sekondari ya ufundi Mtwara.

Nnwele ametaja vifaa atakavyopewa mwanafunzi huyo na ofisi yake kuwa ni sare za shule, viatu, soksi, nguo za michezo, vifaa vya shule, godoro na shuka.

Mkurugenzi huyo alimwagiza Ofisa Maendeleo ya Jamii, Moses Mkoveke, kuharakisha ununuzi wa vifaa hivyo, kumwezesha mwanafunzi huyo kuripoti shuleni kuendelea na elimu ya sekondari.

Pia Nnwele aliziomba taasisi na wadau wengine kuguswa na changamoto zinazomkabili mwanafunzi huyo kwa kumsaidia mahitaji mbalimbali aweze kutimiza ndoto yake kutokana na kufiwa na baba yake mzazi.

Somoe Issa, mama mzazi wa mwanafunzi huyo, alimshukuru mkurugenzi huyo kwa msaada aliompatia kwa kuwa uwezo wake wa kumsomesha ulikuwa umefikia ukingo-

# RC aagiza ujenzi kufanyika saa 24

**Na Julieth Mkireri,** KIBITI

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, amemwagiza mkandarasi anayejenga daraja la Mbuchi, lililoko Kibiti kuhakikisha anafanya kazi saa 24 ili kuharakisha ujenzi na kurahisisha usafiri kwa wananchi.

Kunenge alitoa agizo hilo jana alipotembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi na kwamba kutokana na kazi ya kufunga daraja inayoendelea sasa, mkandarasi anayejenga daraja hilo kwa kushirikiana na Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA) wanatakiwa kufanya kazi muda wote.

"Hakikisheni hatuongezi muda, fanyeni kazi usiku na mchana daraja hili likamilike kwa wakati muwaondolee kero hawa wananchi wanaoteseka," alisema Kunenge.

Alisema daraja hilo ni la tatu kwa ukubwa katika mkoa wa Pwani likiongozwa na la Wami na Ruvu ambalo likikamilika litafungua fursa za kiuchumi na uwekezaji.

"Maagizo yangu tunapokuwa tunatekeleza mradi wowote wa maendeleo wataalamu watachukuliwa kutoka taasisi yoyote ya serikali ili mradi ukamilike kwa wakati," alisema. Kunenge alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kufungua nchi kwa ujenzi wa miundombinu ikiwamo Mkoa wa Pwani kupitia madaraja mbalimbali na barabara zinazojengwa kuwawezesha wananchi kusafirisha bidhaa zao kwa urahisi.

Naye Meneja wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mjini (TARURA) mkoa wa Pwani, Mhandisi Leopold Runji, alisema utekelezaji wa mradi huo unafanywa na Mkandarasi Alfa Logistics ya Tanzania kwa gharama ya Sh. bilioni 6.1, mradi ambao ulitazamiwa kuchukua miezi 12 kuanzia Januari 2021.

Alisema mkandarasi anayejenga daraja la Mbuchi lenye urefu wa mita 61 na ameomba kuongezewa wiki 23 akiainisha sababu kuwa ni mvua kupita kiasi iliyosababisha mafuriko.

Alisema kwa kuzingatia hali hiyo, Mhandisi mshauri alimshauri Meneja wa TARURA kumwongezea mkandarasi wiki sita kumalizia kazi ndogo ndogo baada ya kufunga chuma za daraja hilo.

Runji alisema daraja hilo linatarajia kukamilika mwezi Februari, mwaka huu na ufungaji wa daraja la chuma umehusisha wataalamu kutoka TARURA makao makuu, TARURA mkoa, Tanroads na wananchi wa vijiji vya jirani.

"Kazi ya ufungaji wa daraja ilianza Januari 10 na unatarajiwa kukamilika Januari 23 kwa gharama ya Sh. milioni 67, kazi ambayo inafanywa na wataalamu kutoka TARURA.

Kwa mujibu wa meneja huyo, mradi unajumuisha ujenzi wa maegemeo mawili ya daraja la Mbuchi lenye urefu wa mita 61, barabara mkaribio mita 400 (mita 200) kwa kila upande, maboresho ya barabara kilomita 23 kutoka Mohoro hadi Mbuchi.

Mmoja wa wakazi wa Kata ya Mbuchi, Hassan Yusuph aliishukuru serikali kwa ujenzi wa daraja hilo ambalo ilikuwa kilio cha kwa zaidi ya miaka 60.

Yusuph alisema kabla ya ujenzi wa daraja hilo walikuwa wakivuka kwa mitumbwi ambayo wakati mwingine ilikuwa inazama na kusababisha vifo.

Alisema kila mwaka hususan kipindi cha masika wapo watu walikuwa wakipoteza maisha wakati wa kuvuka ikiwa ni pamoja na kupoteza mazao yao ya nazi wakiwa wanazipeleka sokoni.




# HABARI PICHANI



Wafanyabiashara wakiangalia kwa mbali vibanda vyao vilivyoteketea.



Mmoja wa wafanyabiashara akiwa na ndoo akitoka kukagua eneo la mabanda yaliyoteketea kwa moto.



Askari wa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji wakiwa wanapambana kuuzima moto katika soko la Ilala Mchikichini jijini Dar es Salaam, jana.



Wafanyabiashara wakiondoa baadhi ya bidhaa zilizosalimika kwenye janga la moto.



Baadhi ya wafanyabiashara wakiwa na sehemu ya mali zao zilizookolewa. **PICHA ZOTE: JUMANNE JUMA**

HABARI KITAIFA

# RC Shinyanga ahamasisha wananchi chanjo UVIKO-19

Na Marco Maduhu, KAHAMA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, amewasisitiza wananchi mkoani humo kujitokeza kwa wingi kupata chanjo ya UVIKO-19 ili kujikinga, kuendelea kuwa salama watakapoambukiwa ugonjwa huo.

Mjema alibainisha hayo kwa nyakati tofauti mwishoni mwa wiki wakati wa mikutano ya hadhara wilayani Kahama ya kusikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi, ukaguzi wa miundombinu ya barabara, pamoja na kutembelea walengwa wa mfuko wa kusaidia kaya maskini (TASAF).

Alisema moja ya silaha ya kupambana na maambukizi ya virusi vya ugonjwa huo ni kupata chanjo ya UVIKO-19, ambayo itamlinda mtu endapo akipata virusi hivyo na kutopata madhara makubwa, tofauti na yule ambaye hakupata chanjo kabisa.

"Ndugu zangu wananchi wa Kahama na mkoa mzima wa Shinyanga, napenda kuwasisitiza jitokezeni kwa wingi kwenye huduma za afya na kupata chanjo ya UVIKO-19, ili kupata kinga zaidi ya kutodhurika na virusi vya Corona," alisema Mjema.

"Kama mtu akiwa amepata chanjo hii ya UVIKO, siku akiambukizwa virusi vya corona hawezi kupata madhara makubwa na atapona tu, lakini yule ambaye hakupata chanjo maisha yake yatakuwa hatarini, hivyo jitokezeni mpate chanjo kwa kulinda maisha yenu," aliongeza.

Mjema alisema katika suala la kulinda watoto dhidi ya corona shuleni, Rais Samia Suluhu Hassan, alitoa fedha za ujenzi wa vyumba vya madarasa kupitia fedha za UVIKO-19, ili wasisome kwa kubanana madarasani na kuagiza wakuu wa shule wahakikishe ndoo za majitiririka zinakuwapo kwa kila darasa.

Katika hatua nyingine, aliwataka wazazi kupuuza maneno ya upotoshaji kuwa kuanzia shule za awali hadi kidato cha nne ada zimerudi, na kusisitiza elimu ni bure na wawapeleke watoto wao shule ili watimize ndoto zao.

Pia alitoa onyo kwa wanaume wanaoendekeza tabia ya kufanya mapenzi na wanafunzi na kuwapa mimba za utotoni kuwa atakayekamatwa, serikali itamchukulia hatua kali za kisheria.

Aliwataka wanafunzi wanapokuwa wakirubuniwa au kutaka kuozeshwa ndoa za utotoni, watoe taarifa kwa viongozi au dawati la jinsia la polisi, ili hatua za haraka zichukuliwe kabla ya kupata madhara na kuharibu ndoto za maisha yao.

Katika mikutano hiyo ya hadhara, Mkuu huyo wa Mkoa alitatua kero mbalimbali pamoja na zingine kuwaachia wataalamu, ikiwamo ya migogoro ya ardhi, kesi za jinai, na utoaji wa huduma mbovu za matibabu kwenye zahanati na vituo vya afya.

Akizungumzia utatuzi wa miondombinu mibovu ya barabara, alisema serikali mkoani humo imepata Sh. bilioni 1.5 fedha za tozo za mafuta, na kumpa Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA), ili kukarabati maeneo ya barabara ambayo ni korofi.

Naye Mbunge wa Msalala, Idd Kassim, alisema katika ujenzi wa miundombinu ya barabara kwenye maeneo ambayo yanazungukwa na mgodi wa dhahabu Bulyanhuru, tayari wapo kwenye mazungumzo ya hatua za mwisho, ili ujenzi wa barabara hizo uanze mara moja kwa kiwango cha lami.

Nao baadhi ya wananchi waliotoa kero zao, nyingi zilikuwa ni migogoro ya ardhi, huduma mbovu za afya kwa kuambiwa hakuna dawa na kuelekezwa kununua kwenye maduka ya watu binafsi.

Kero zingine ni wananchi wenye bima CHF kutopewa huduma stahiki, wazee kukosa matibabu bure, utozwaji wa fedha kuandikisha wanafunzi, ubovu wa barabara, pamoja na vijana wazawa kukosa ajira kwenye mgodi wa dhahabu Bulyanhuru.



Diwani wa Kata ya Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, Salome Mnyawi, akisoma taarifa ya mafanikio na changamoto za kata yake kwenye kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika Mji Mdogo wa Orkesumet, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# DAWASA yaongezewa eneo la kuhudumia

Na Frank Monyo

WIZARA ya Maji imetangaza kuongeza eneo la kihuduma kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), kwa kutekeleza mradi wa maji Kazimzumbwi hadi Masaki kwenye kata ya Kazimzumbwi wilayani Kisarawe, mkoani Pwani ili kusogeza huduma ya maji kwa wakazi wa maeneo hayo.

Uamuzi huo umekuja baada ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, ambaye ni Mbunge wa Kisarawe kutoa ombi kwa Wizara ya Maji kuipa DAWASA jukumu la kupeleka maji kwenye mradi huo utakaonufaisha kata za Kazimzumbwi, Masaki, Msimbu, Kibuta na Marumbo wenye urefu wa kilomita 192 baada ya RUWASA kushindwa kutekeleza kutokana na ufinyu wa bajeti.

Akitangaza uamuzi huo kwa mujibu wa Sheria ya Maji sura namba tano jana, Waziri wa Maji Jumaa Aweso, amewataka DAWASA kufikisha huduma ya maji kwenye eneo hilo kutoka kwenye mradi wa maji Kibamba - Kisarawe.

"DAWASA mkae na wataalamu wa RUWASA ili mje na utaratibu wa namna ya kutekeleza mradi huu," alisema Aweso akiwa kwenye ziara ya kutembelea mradi wa maji Kibamba - Kisarawe.

"Kata za Kazimzumbwi, Masaki, Msimbu, Kibuta na Marumbo ni maeneo yenye changamoto ya maji kwa muda mrefu ambayo haijapata utatuzi," alisema Aweso.

Waziri Jafo alipongeza DAWASA kwa kazi kubwa ya kutekeleza mradi wa maji Kibamba - Kisarawe kwa Sh. bilioni 10.6 kwa Wilaya ya Kisarawe, ambayo imesaidia kuimarisha upatikanaji wa maji kwa wananchi wa Kisarawe.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Cyprian Luhemeja, alikubali kupokea jukumu hilo na kuahidi kutekeleza mradi huo ndani ya muda muafaka ili wananchi wa kata za Kazimzumbwi, Masaki, Msimbu, Kibuta na Marumbo, waweze kunufaika na mradi. Mradi wa maji Kibamba - Kisarawe unazalisha lita milioni sita za maji kwa siku ambayo ni zaidi ya mahitaji ya maji kwa Wilaya ya Kisarawe ambayo ni lita milioni 1.2.

# TASAF yalipa bil. 9.2/- kaya maskini

Na Ashton Balaigwa, MOROGORO

KAYA 41,247 zilizoko kwenye Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mkoa wa Morogoro, zimelipwa jumla ya Sh. bilioni 9.2 katika madirisha sita kuanzia Julai- Agosti, 2020 hadi Mei –Juni, 2021.

Mratibu wa TASAF Mkoa wa Morogoro, Jacob Kayange, alisema hayo wakati wa ziara ya wajumbe wa Bodi ya Kamati ya Taifa ya Uongozi wa Mfuko huo uliotembelea mkoani hapa.

Alisema malipo ya awamu ya tatu yamefanyika tangu kuzinduliwa kwa mpango wa kunusuru kaya maskini katika kipindi cha pili cha utekelezaji wa TASAF III, Februari 17, 2020 uliofanywa na hayati Rais Dk. John Magufuli.

Kayange alisema jumla ya Sh. bilioni 10.2 zimepokelewa kati ya hizo Sh. bilioni 9.2 kwa ajili ya malipo ya kaya 41,247 zilizoko katika mpango na Sh. milioni 927.8 kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa mpango ngazi ya kijiji, kata, halmashauri na mkoa.

Alisema mpango wa TASAF awamu ya tatu umelenga kuziwezesha kaya hizo ili kuondokana na umaskini uliokithiri na kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji ya msingi ya kimaisha yanayojumuisha chakula, elimu na afya.

Katika hatua nyingine, mpango wa kuweka akiba na kuwekeza katika mkoa huo ulioanza kutekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa umewezesha kuundwa kwa vikundi 428 vyenye jumla ya wanachama 5,860 na kujiwekea akiba ya Sh. milioni 93.1.

Mratibu wa mkoa wa Mfuko huo, alisema fedha hizo wamekuwa wakizitumia kwa kuanzisha shughuli za kujiongezea kipato zikiwamo shughuli za kilimo, ufugaji, ushonaji na kilimo cha mboga na biashara ndogo.

Nao baadhi ya wanufaika wa TASAF katika Kijiji cha Mkambarani, Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro akiwamo Edna Cham, alisema wameshaunda vikundi sita vinavyo shughulika na ujasiriamali.

Alisema kupitia vikundi hivyo, wanachama wamenufaika kujikwamua kiuchumi kutokana na kutengeneza sabuni na bidhaa za aina nyingine katika vikundi vyao.

"Sisi kikundi chetu cha Furaha, tunaweza kulipia ada za watoto wetu pamoja na sare za shule na michango mingine ikiwamo chakula cha watoto," alisema Edna.

# Mradi kuchunguza upya kesi ukatili kijinsia waanza

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, limeanzisha mpango maalumu wa kuzipeleleza upya kesi zilizokosa ushahidi za ubakaji na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto ili wazifufue na kuzirudisha upya mahakamani, kuzitafutia ufumbuzi na wahusika wawajibishwe kisheria.

Mpango huo unatekelezwa katika kata 26 za Halmashauri Wilaya ya Shinyanga kati ya Januari hadi Machi, mwaka huu, kwa Shilingi milioni nane zilizotolewa na Mfuko wa Ruzuku wa Wanawake Tanzania (WFT), ili kukomesha vitendo vya namna hiyo ndani ya jamii.

Mkuu wa Dawati la Jinsia mkoani Shinyanga, Analyse Desdery, alisema hayo juzi wakati wa ufunguzi wa mradi wa uratibu na ufuatiliaji wa afua za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWWA), uliofanyika Kata ya Iselamangazi, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

Alisema, wamepokea mradi wa nafasi ya dawati la jinsia katika kutekeleza sheria zinazomlinda mwanamke na mtoto na wataanza kwa kutoa elimu ya mabadiliko ya sheria kwa mawakili ambao sio wa kiserikali na askari wa dawati la jinsia ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa kesi.

Desdery alisema, watazichunguza upya kesi za ubakaji na ukatili wa kijinsia zilizokosa ushahidi na kuzirejesha upya mahakamani na mpaka sasa wanakesi 16 ambazo zinahitaji kufanyiwa uchunguzi na kupata matokeo chanya, na kuwataka wananchi na wadau kutoa ushirikiano wao.

"Huwezi kupata matokeo ya upelelezi wa kesi hizi kwa mwezi mmoja, zoezi hili tutaendelea kulifanya hata kama mradi utakuwa umekwisha muda wake Machi mwaka huu...Vitendo vya namna hii vimekuwa vikikwamisha malengo ya wanafunzi wetu na kunyanyasa wanawake," alisema Desdery.

Pia alisema watatoa elimu za ukatili katika kata 26 za halmashauri hiyo hasa kata zenye matukio mengi ya ukatili ili wananchi watambue njia gani wanatakiwa kuanza kutoa ripoti za matukio hayo, kesi nyingi zinakosa ushihidi baada ya aliyebakwa kuoga kabla ya kufanyiwa vipimo.



Mkazi wa Iringa Mjini akipita nje ya ofisi za Halmashauri ya Manispaa akiwa na mzigo wa kuni alizotoka kuchanja kwenye pori la msitu wa asili wa Gangilonga, jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# TBS yaelimisha wazalishaji, wasambazaji bidhaa

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limetoa elimu ya viwango kwa wazalishaji, wasambazaji, waagizaji wa bidhaa nje ya nchi na wafanyabiashara visiwani Zanzibar.

Elimu hiyo ilitolewa wakati wa tamasha la nane la biashara Zanzibar lililofanyika kuanzia Januari 2 na kumalizika Januari 15, mwaka huu visiwani humo.

Tamasha hilo lilifunguliwa na Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman.

Akizungumza wakati wa tamasha hilo, Ofisa Masoko TBS, Rhoda Mayugu, alisema shirika limetumia tamasha hilo kutoa elimu kuhusu majukumu yake ambayo ni pamoja na uthibitishaji wa bidhaa na mifumo, usajili na

majengo na bidhaa za chakula na vipodozi, upimaji, uandaaji wa viwango na udhibiti wa bidhaa kwa bidhaa zinatoka nje ya nchi.

"TBS ni shirika lililopewa dhamana ya kusimamia ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini na zile zinatoka nje ya nchi hivyo basi wazalishaji, wasambazaji, waagizaji wa bidhaa nje ya nchi na wafanyabiashara wanatakiwa kuhakikisha bidhaa wazaozalisha na zile zinazotoka nje ya nchi zimethibitishwa na kukidhi matakwa ya viwango kabla ya kuingizwa sokoni," alisema Mayugu.

Aliongeza kuwa wananchi kama watumiaji wa bidhaa wana nafasi kubwa ya kuhakikisha bidhaa zilipo sokoni zimekidhi matakwa ya viwango, na kuwa wao ndiyo wanofanya uamuzi wa kununua au kutokununua bidhaa.

"Wananchi kama watumiaji wa mwisho wa bidhaa ndiyo waathirika wakubwa wa bidhaa hafifu na endapo watajenga utamaduni wa kununua bidhaa zile tu ambazo zimethibitishwa ubora ni wazi soko la Tanzania litakuwa na bidhaa zilizokidhi matakwa ya viwango na kama taifa tutakuwa tumeshinda vita ya bidhaa hafifu," alisema Mayugu na kuongeza;

"Jukumu la kuhakikisha Tanzania inakuwa na bidhaa zilizokidhi matakwa ya viwango si la TBS pekee, bali ni la kila Mtanzania kuanzia mzalishaji wa bidhaa, mwagizaji wa nje ya nchi, msambazaji, muuzaji na mtumiaji wa bidhaa," alisema.

"Kwa hiyo katika kutimiza lengo hilo kwenye tamasha hili tuliwaelimisha kuhusiana na alama ya ubora. Wanatakiwa kujua kwamba bidhaa zote ambazo zimethibitishwa ubora huwa zinatumia alama ya ubora," Mayugu.

# Watakaoshindwa kupeleka watoto shule kukamatwa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MKUU wa Wilaya ya Kilosa, mkoani Morogoro, Alhaji Majdi Mwanga, amesema atawakamata na kuwafikisha mahakamani wazazi na walezi watakaoshindwa kuwapeleka shuleni watoto wao waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza leo.

Alhaji Mwanga alisema hayo mjini Kilosa katika mkutano wa hadhara na wananchi kuhusu uhamasishaji shughuli maendeleo ikiwamo sekta ya elimu.

Alisema ili kuona watoto waliochaguliwa kidato cha kwanza wanaingia madarasani leo, ofisi yake imeandaa mikataba kati ya wazazi, walezi kuhusu kudhibiti tabia ya baadhi ya wazazi kuwa chanzo cha wanafunzi kukatisha masomo.

Alisema hatua hiyo ni kutekeleza ibara ya 11 (2) na (3) ya Katiba inayosisitiza haki ya msingi ya kupata elimu.

"Tumeshatayarisha mikataba ambayo inalenga kuimarisha usimamizi kwa wazazi na walezi, kutimiza wajibu wa malezi kwa watoto wao na ilishasambazwa katika shule za sekondari na ofisi za serikali za vijiji na Kata," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kilosa, Ameir Mbaraka, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuiwezesha Wilaya ya Kilosa Sh. bilioni 4.3 zilizotumika kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa 186.

Naye Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya wilaya hiyo, Kisena Mabuba, alisema halmashauri hiyo imepangiwa wanafunzi 9,405 ambao wanatarajia kuanza masomo ya kidato cha kwanza Januari 17, mwaka huu.

Mabuba alisema mpango mwingine ni kuhamasisha uandikishwaji wanafunzi wa awali na darasa la kwanza kutoka kwenye jamii za wafugaji.

"Nawataka jamii ya wafugaji wajitokeze kuwaandikisha watoto wao waliofikia umri wa kuanzishwa shule ili waepuke mkono wa sheria," alisema Mabuba.

Alisema halmashauri itaendeleza mchakato kusajili shule shikizi, ili kutoa fursa kwa wanafunzi wa shule za msingi kuondokana na ulazima wa kutembea umbali mrefu.

Nao baadhi ya wakazi wa Kijiji cha Gezaulole, wilayani humo, Everine Mlinga, alisema wengi wa wazazi na walezi wamekwishafikiwa na mikataba hiyo na hakuna ugumu katika utekelezaji wake.

Nipashe
Spotika



JINSI RASHFORD ANAVYOWEZA KURUDISHA KIWANGO MAN UTD UK. 12 - 13




MBAPPE

# WASHAMBULIAJI WATANO BORA WA KUSHOTO 2021

**LONDON,** Uingereza

TAYARI tumepitia nafasi nyingi za uwanjani kwa mchezo nzuri kabisa wa mpira wa miguu duniani.

Makipa, mabeki wa kati, viungo wa ulinzi, viungo wa kati, washambuliaji wa kati na mabeki wa kushoto, lakini sasa orodha yetu tunaangalia washambuliaji wa kushoto.

Hivi sasa tutaeleza kwa undani baadhi ya washambuliaji bora wa upande wa kushoto kwenye mchezo huu; nyota wanaotengeneza mabao na kuwatengenezea wenzao kiurahisi.

Je, unahitaji kukumbushwa jinsi mchakato mzima unavyofanya kazi? Hapa ndio unahitaji kujua. Mwanasoka wa kiwango cha kimataifa anafafanuliwa kama mmoja wa wachezaji watano bora duniani katika nafasi zao.

Hapa tunaangalia takwimu za StatsPerform katika kipindi cha Januari 1, 2021 hadi Novemba 30, 2021, twende sasa...

### #5. VINICIUS JR

Vinicius Jr daima amekuwa mchezaji mwenye kipaji cha ajabu, lakini katika misimu yake ya kwanza nchini Hispania alionekana mbichi, asiye na uwezo na aliyekosa kitu fulani.

Hayo yote yalibadilika alipofikisha umri wa miaka 21 mnamo Julai mwaka jana. Alirejea kutoka Copa America (ambako aliiwakilisha Brazil kwa mara ya kwanza katika muda wa miezi 18) akiwa mchezaji tofauti kabisa, akipiga mashuti bila kusita.

Akiwa na mabao 12 na asisti tisa katika mechi 24 za kwanza za Real msimu huu, na kama mchezaji wa kimataifa wa Brazil, amepiga hatua inayofuata ambayo wengi hawana. Kidogo cha kutisha? Bado ana miaka 21. Kunaweza kuwa na mengi zaidi yajayo.

### #4. LEROY SANE

Msimu wa kwanza wa Leroy Sane kule Bayern Munich unazingatiwa na wengi kuwa haukuwa mzuri kwa Mjerumani huyo. Hakika, wengi walimtarajia kuwa juu zaidi kutokana na kipaji chake.

Kuanzia mwanzo wa mwaka, winga huyo wa zamani wa Manchester City amekuwa katika kiwango cha juu na cha kuvutia, akielekea kileleni katika msimu wa 2021/22.

Sane anarejea kwenye ubora wake na tayari amelingana na mchango wake wa mabao kutoka msimu uliopita. Ikiwa anaweza kuendelea, ni nani anayejua miezi 12 ijayo?

### #3. SON HEUNG-MIN

Baada ya uchezaji wa mshambuliaji wao msimu wa majira ya joto, Tottenham ilimhitaji Son Heung-min kuongeza kasi na akawa kivutio chao na ndivyo alivyofanikiwa kufanya.

Sasa ni mchezaji muhimu wa Spurs wanapokuwa kwenye matatizo, Son anasifika kwa umahiri wake bora - akifunga asilimia 14.6% ya mashuti yake - huku pia akiwa ametengeneza nafasi nyingi zaidi (84).

Raia huyo wa Korea Kusini anastahili kuwa kwenye orodha hii ya washambuliaji wa kushoto kwa wakati huu.

### #2. SADIO MANE (CHINI 1)

Liverpool wamekuwa na wakati mgumu uliopita au zaidi baada ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England msimu wa 2020/21, lakini wamerejea wakiwa na nguvu mwaka huu na Sadio Mane bado ni muhimu kama zamani.

Nyota huyo wa Senegal anabaki kuwa chanzo cha kutegemewa cha mabao kwa 'wekundu' hao - akifunga mara moja kila baada ya dakika 188 - na uwapo wake katika kipindi cha mwaka mmoja ambapo kikosi chake kilipunguzwa na majeraha kilimfanya kuwa wa thamani zaidi.

Ubora wa Mane kwenye safu ya mbele ya Liverpool unamfanya kuwa mmoja wa washambuliaji hatari zaidi katika soka la dunia kwa sasa.

### #1. KYLIAN MBAPPÉ


Hatuwezi kushangaa sana kuona huyu akiibuka kinara kwenye orodha hii.

Hii ni kwa sababu Kylian Mbappé amekuwa mmoja wa washambuliaji wenye kasi zaidi anapotokea kushoto na hufunga kirahisi zaidi.

Kwa upande wa ufungaji mabao, hakuna mshindani hata mmoja kwa Mfaransa huyo kwa wanaotokea kushoto na sasa ana mabao yake tisa kibindoni kwenye Ligi Kuu Ufaransa. Pia anaongoza kwa kikosi hicho cha PSG.

## ISIKUPITE

Kwa kipindi hiki cha Januari, Vinicius Junior wa Real Madrid ndiye mchezaji mwenye thamani kubwa zaidi euro milioni 166.4, akifuatiwa na Phil Foden (Manchester City) euro milioni 152.6 na Erling Haaland wa Borussia Dortmund euro milioni 142.5, kwa mujibu wa International Center for Sports Studies (CIES).



# JINSI RASHFORD ANAVYOWEZA KURUDISHA KIWANGO MAN UTD



RASHFORD

**MANCHESTER,** England

ZUNGUMZA na watu wanaomfahamu Marcus Rashford wanakubali kwamba, mshambuliaji huyo wa Manchester United anasumbuliwa na hali ya kutojiamini.

**Makala haya kutoka BBC Sport yanachambua kwa kina namna Rashford anavyoweza kurudi kwenye kiwango chake. Hii inatokana na kushuka kwa kiwango chake cha mchezo kwa misimu michache iliyopita, ambayo, kwa sasa, haipunguzwi na mtiririko wa kawaida wa mabao.**

Kiwango chake cha kukatisha tamaa wakati Man United ilipoilaza Aston Villa bao 1-0 kwenye mchezo wa Kombe la FA Jumatatu iliyopita, kiliwafanya wachambuzi wengi kukuna kichwa.

“Sitaki kumtaja Marcus Rashford peke yake kwa sababu hatujui kinachoendelea ndani kwake,” alisema Alan Shearer wakati wa uchambuzi wa mchezo huo. “Lakini kila kitu kinaonekana kuwa ni juhudi za kweli kwake. Anaonekana hayupo sawa kabisa.”

“Anaonekana kuvunjika moyo,” aliongeza mshambuliaji wa zamani wa Manchester United, Dion Dublin wakati wa matangazo hayo. “Sijamwona akitabasamu kwa muda mrefu.”

Tofauti na siku zake za mwanzo kama mchezaji wa kikosi cha kwanza cha United ambapo alionekana kuwa na umuhimu mkubwa.

Ilikuwa Februari 2016 alipoingia uwanjani akiwa na umri wa miaka 18 na kufunga mabao mawili kwenye mechi yake ya kwanza ya Ligi ya Europa dhidi ya Midtjylland ya Denmark.

Siku tatu baadaye, alifunga bao lake la kwanza la Ligi Kuu dhidi ya Arsenal na akapiga mengine mawili.

Kiwango chake kilichangia Rashford kuitwa kwenye kikosi cha England kwenye michuano ya Euro 2016 na kuanza kwake kuichezea timu hiyo kulimfanya afikishe mechi 46, na kucheza kwenye michuano mikubwa mitatu.

Misimu yake miwili kamili ya mwisho ndani ya United imekuwa na matokeo mazuri, huku mabao 43 yakimfanya kuwa na jumla ya mabao 88 katika klabu hiyo mwishoni mwa msimu uliopita.

Hata hivyo, alishindwa kuanza msimu huu baada ya kufanyiwa upasuaji wa bega na hajafunga katika mechi 11 zilizopita, tangu waliposhinda 3-0 dhidi ya Tottenham Oktoba 30, 2021.

Bado ana mabao tisa ili afikishe 100 hapo United na kwa kiwango chake cha sasa, hakuna uhakika kama anaweza kuyafikisha msimu huu.

Na mashabiki wa United wameanza kunung’unika huku matatizo ya Rashford yakifanana na ya timu yao.

## KUJIAMINI

Kujiamini kumekuwa suala kubwa kwa Rashford. Maamuzi ya uwanjani aliyoyafanya hapo awali bila kikwazo sasa hayafikiwi kwa urahisi.

Rashford ametakiwa kurejea katika misingi, kufuata mbinu iliyomletea sifa mwanzo; kukimbia kwa wapinzani kwa kasi yake ya umeme na kuwazidi akili.

Inaonekana rahisi sana. Lakini kwa ujumla kwake ni jambo gumu sana.

## MSAADA

Wachezaji wa zamani na wachambuzi wakati mwingine wanaweza kudharau linapokuja suala la usimamizi wa ‘mkono karibu na bega’ na kupendelea mtindo wa mapenzi magumu waliyozoea kupewa wao kwenye malezi ya makuzi kwenye soka.

Lakini dunia imebadilika. Rashford hahitaji kujisafisha mwenyewe. Anachohitaji, inahisiwa, ni uhakikisho na mwongozo.

BBC Sport imeambiwa, yeye ndiye wa mwisho kufanya mahojiano yaliyopangwa kwa wachezaji, kwa sababu hukaa muda mrefu kwenye uwanja wa mazoezi akifanyia kazi mchezo wake au kufanya mazoezi ya kupiga mashuti na chenga.

Mshambulizi huyo alielewana vema na kocha wa zamani wa United, Ole Gunnar Solskjaer.

Lakini raia huyo wa Norway hakuwa na tabia ya kufundisha sana, kwa hivyo Rashford hakuwahi kujifunza ipasavyo silika za uwindaji za mshambuliaji mwenzake.

Kwa hiyo Rashford akashusha pumzi ndefu, akashinda aibu yake ya asili na akaenda kwa Solskjaer kumwambia kuwa hana uhakika na kile alichokuwa akiulizwa.

Alisema alihisi kiwango chake kimeshuka kwa sababu alikuwa akiombwa kucheza katika majukumu mengi tofauti. Rashford aliambiwa aache kulalamika.

Ralf Rangnick, ambaye alichukua nafasi ya Solskjaer kwa muda mapema Desemba, analenga kuzungumza na wachezaji wake kila baada ya wiki kadhaa. Rashford anahisi Mjerumani huyo anaweza kumsaidia.

Lakini, kama ilivyo kwa kikosi cha United kwa ujumla, kuna sintofahamu juu ya siku zijazo.

Kazi ya Rangnick ni kuleta utulivu wa msimu na kushauri juu ya kuleta mbadala wa kudumu katika msimu wa majira ya joto unaokuja.

Chini ya hali hiyo, si rahisi kuanzisha muunganiko unaohitaji ili kuunda uelewa wa pamoja wa wachezaji wa kikosi hicho.

## NAFASI BORA KWAKE

Rashford anaamini kuwa nafasi yake yenye ufanisi zaidi iko upande wa kushoto, akikatizia huko kusonga mbele.

Hata hivyo, ameshindwa kuipata nafasi hiyo hapo United, kwanza chini ya Solskjaer na sasa chini ya Rangnick.

Akiwa fiti, Paul Pogba amekuwa na tabia ya kuikalia nafasi ya upande wa kushoto, ambayo inaweza kuonekana kama inamfurahisha zaidi mchezaji ambaye moyo wake haupo Old Trafford huku akiwa na uwezo wa kuwajibika linapokuja suala la kusaidia ulinzi.

Msimu uliopita, hii ilimaanisha Rashford sasa atatumika kama mshambuliaji wa kati au upande wa kulia. Ujio wa Cristiano Ronaldo ulibadilisha hali hiyo. Na tangu kuwasili kwa Rangnick, mbinu zimebadilika pia.

Kupitia mabadiliko hayo yote, Rashford amekuwa akicheza cheza tu.

Aliweka mguu wake chini majira ya joto na kudai aruhusiwe kufanyiwa upasuaji wa bega ili kutibu tatizo lililokuwa likimletea usumbufu wakati Solskjaer alipokuwa na shaka.

Ilimaanisha kuwa alirejea katika utimamu wake Oktoba wakati ambapo United ilianza kudorora.

Rashford alifunga mara tatu katika mechi zake saba za kwanza msimu huu, lakini ndani ya kipindi hicho wakafungwa nyumbani na Liverpool na Manchester City na kipigo cha ugenini kwa Watford ambacho kilimaliza muda wa Solskjaer kuwa kocha hapo Old Trafford.

Rangnick aliingia na mara moja akaanzisha mfumo wake wa 4-2-2-2, ambao hupata upana wake kutoka beki za pembeni.

Ni dhidi ya Villa pekee ambapo Mjerumani huyo alitumia mfumo wa Solskjaer wa 4-2-3-1, huku Rashford akiwa katika nafasi yake ya upande wa kushoto.

Uchezaji wake dhidi ya Villa, dhahiri, haukuwa mzuri. Hata hivyo, ikizingatiwa hii ilikuwa nafasi ya tano tofauti ambayo Rashford amecheza katika mifumo minne tofauti msimu huu, labda asamehewe kwa kutokuwa kwenye ubora wake.

## POCHETTION ATAMSAIDIA?

Kuna hisia kwamba hali ya sasa ya Rashford inaweza kutatuliwa haraka sana.

Amedhamiria kuanza tena kufunga mabao. Na imesisitizwa kuwa hakuna tatizo hapo United kuhusu kazi yake nje ya uwanja karibu na watoto wasiojiweza, ambayo, kwa vyovyote vile, haijawa muhimu sana katika maisha yake msimu huu.

Hata hivyo, Rashford angefaidika kutokana na mwelekeo wa wazi zaidi - na fursa ya kufanya kazi na kocha anayemwamini.

Ikizingatiwa Mauricio Pochettino ni shabiki aliyethibitishwa, United ikimchukua raia huyo wa Argentina kuchukua nafasi ya Solskjaer kama kocha wa kudumu msimu wa joto, itakuwa habari njema kwa Muingereza huyo.

Kwa sasa, Rashford ataendelea na kazi, kufanya mazoezi yake ya ziada na anatumaini kuwa kiwango chake kitabadilika haraka inavyowezekana.

## Nukuu

“Nilipomwona [Clatous] Chama kupitia video mbalimbali, nilikubali uwezo wake na ndio maana sikutaka kuweka kikwazo katika kurejea kwake. Ni mchezaji mzuri sana, naamini ataisaidia timu kwa kushirikiana na wenzake, uwezo anao mkubwa na nina imani naye, angekuwa mchezaji wa kawaida asingezungumzwa kiasi kile, ilinifanya hata mimi kumfuatilia sana ili kuona uwezo wake,” **Kocha wa Simba, Pablo Franco.**



“Nadhani kiwango cha uchezaji kilikuwa bora zaidi kuliko matokeo kwa uhakika. Pengine kutawala zaidi. Tulitawala mchezo vizuri zaidi kuliko hapo awali. Tunastahili zaidi. Lakini, mchezo sio kustahili, ni kuhusu pointi. Bahati mbaya kwetu. Bado kuna mengi ya kuboresha hata kama kiwango kilikuwa kizuri. Sina furaha hata kidogo,” **Kiungo wa Manchester United, Bruno Fernandes baada ya timu yao kutoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Aston Villa juzi.**



“Tulizungumza kabla ya mchezo, ‘nataka kushinda mechi [dhidi ya Chelsea] kama tutastahili kushinda’ na kama tumestahili, napenda soka ikiwa ni haki. Nilifurahi tuliposhinda dhidi ya Arsenal, lakini hatukustahili kushinda mchezo huo,” **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola baada ya kuifunga Chelsea 1-0 juzi.**





# SIMBA NA REKODI KIBAO KOMBE LA MAPINDUZI

**Na Mwandishi Wetu**

MWAMUZI alipopuliza kipenga cha kumaliza mechi, wanachama na mashabiki wa Simba walilipuka kwa hoi, nderemo na vifijo, kwani timu yao ilikuwa imeshinda bao 1-0 dhidi ya Azam FC kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Mapinduzi, Alhamisi iliyopita katika Uwanja wa Amaan Zanzibar.

Furaha ilizidi kifani pale Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi aliponyanyua kombe hilo na kumkabidhi nahodha, John Bocco kuashiria kuwa ndiyo mabingwa wapya wa michuano hiyo kwa mwaka huu wa 2022.

Lilikuwa ni bao la mkwaju wa penalti, ikiwekwa nyavuni na straika wa Kinyarwanda, Meddie Kagere dakika ya 55, baada ya kiungo machachari raia wa Senegal, Pape Sakho kufanyia madhambi na kipa Mathias Kigonya kwenye eneo la hatari.

Ilikuwa ni michuano iliyofana zaidi kuliko miaka kadhaa iliyopita na kurejea kwenye ubora wake. Timu 10 zilizoshiriki zikishindana kila moja na ubora wake, hadi kupatikana kwa bingwa.

Ziligawanyika katika makundi matatu, A likiwa na timu nne ambazo ni Azam FC na Namungo kutoka Bara na Yosso Boys na Meli Nne City kutoka Zanzibar.

Kundi B liliundwa na timu ya Yanga kutoka Bara, Taifa Jang'ombe na KMKM kutoka Zanzibar, huku Simba ya Bara ikiwa Kundi C pamoja na Selem View na Mlandege za Zanzibar.

Kwenye makala haya tutaangalia rekodi kadhaa ambazo Simba imeweka kwenye michuano hiyo iliyomalizika na hata iliyopita, twende sasa...

### #1. Yatwaa kwa mara ya tatu

Ilikuwa ni mara ya tatu kwa Simba kutwaa ubingwa huo, tangu michuano hiyo ianze kuchezwa mwaka 1998. Imetumia miaka sita hadi kulipata tena tangu 2015 ilipolitwa kwa kuifunga Mtibwa Sugar kwa mikwaju penalti 4-3, na hii ni baada ya suluhu ya dakika 90.

Miaka minne iliyopita kabla ya hapo, Simba iliwahi kutwaa Kombe la Mapinduzi mwaka 2011 kwa kuwaadhibu watani zao wa jadi, Yanga mabao 2-0 kwa mabao ya Patrick Ochan dakika ya 33 na Shija Mkina dakika ya 72.

### #2. Fainali mara tisa

Simba ndiyo timu iliyoingia fainali mara nyingi zaidi kuliko timu yoyote ile kwenye Kombe la Mapinduzi. Imeingia mara tisa, mara tano ikilikosa kombe na mara tatu ikilitwaa.

Ililikosa mwaka 2014 ilipochapwa fainali bao 1-0 dhidi ya KCCA ya Uganda, ikafungwa tena bao 1-0, mechi ya fainali 2017 dhidi ya Azam FC, 2019, ikalikosa tena kwa kufungwa mabao 2-1 dhidi ya Azam FC, 2020 ikadunguliwa bao 1-0 dhidi ya Mtibwa Sugar na mwaka jana, ilifungwa na watani zao wa jadi kwa mikwaju 4-3 ya penalti, baada ya suluhu. Mara tatu iliochukua ni zile zilizoorozeshwa hapo juu.

### #3. Ubingwa bila kuruhusu bao

Imetwaa ubingwa huo msimu huu bila kuruhusu bao, ikiwatumia makipa wake wote wawili, Benno Kakolanya alisimama langoni kwenye mechi ya kwanza na zilizobaki zote akikaa kipa namba moja, Aishi Manula.

Ilianza kampeni yake Januari 5 ilipoichapa Selem View mabao 2-0, yaliyofungwa na Pape Sakho na Rally Bwalya kabla ya kulazimishwa suluhu dhidi ya Mlandege Januari 7. Kwenye mechi ya nusu fainali iliichapa Namungo 2-0 kupitia kwa Kagere na Sakho, kabla ya kuondoka na ushindi wa bao 1-0 kwenye mechi ya fainali, Kagere akienda kambani tena.

### #4. Wachezaji bora mara tatu

Wachezaji wa Simba wamechukua uchezaji bora wa mechi mara tatu kwenye michezo minne ambazo zimechezwa.

Bwalya aliibuka mchezaji bora kwenye mechi dhidi ya Selem View, Sakho akiwa ni mchezaji bora wa mechi dhidi ya Namungo FC, na Henock Inonga naye akipata tuzo hiyo kwenye mechi ya fainali dhidi ya Azam FC.

### #5. Tuzo za kumwaga fainali

Baada ya mechi ya fainali, ikakomba asilimia zaidi ya 90 ya tuzo zote za michuano hiyo, ikianza kwa kipa bora kuwa ni Manula. Mbali na Inonga kuchaguliwa kuwa mchezaji bora wa mechi, lakini Sakho alichaguliwa kuwa ndiye mchezaji bora wa michuano hiyo mwaka huu na Kagere kuwa mfungaji bora.

## JE, WAJUA?



KWA mwaka 2021, Bondia Conor McGregor ndiye mwanamichezo aliyekuwa akilipwa fedha nyingi zaidi kwa dakika akiwa anaingiza dola milioni 8.6, kwa mujibu wa Forbes huku akifuatiwa na bondia Canelo Alvarez dola 444,000 kwa dakika wakati mchezaji wa mpira wa kikapu wa Marekani, Tom Brady akishika nafasi ya tatu kwa kuingiza dola 37,000 kwa dakika.






Kinamama wa Kijiji cha Msembeta wilayani Bahi wanaojishughulisha na ujasiriamali wakiwauzia wateja wao nyanya barabara kuu ya Dodoma na Singida, ndoo moja kwa shilingi 5,000 jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Silinde akumbusha ratiba za masomo kuzingatiwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, amewataka wasimamizi wa walimu, kuhudhuria darasani kila siku kulingana na ratiba za masomo zilivyopangwa ili kuepuka kuathiri utekelezaji wa kalenda ya mitaala.

Silinde, alibainisha hayo juzi jijini Dodoma alipokuwa akifunga mafunzo ya kalenda ya utekelezaji wa mitaala kwa shule za msingi na sekondari kwa maofisa elimu mikoa, maofisa taaluma mikoa na wathibiti wakuu wa ubora wa shule kanda.

Alisema hatua hiyo itasaidia utekelezaji wa kalenda hiyo.

Vile vile, alisema kalenda ya utekelezaji wa mitaala inakwenda sambamba na upatikanaji wa matumizi sahihi ya vitabu vya kiada na ziada.

"Naamini kuwa shule zote zina vitabu vya kutosha na vingine vinaendelea kusambazwa na Taasisi ya Elimu Tanzania. Naomba kuwakumbusha kwamba vitabu hivyo ni msaada mkubwa kwa wanafunzi, huvitumia kupata ufafanuzi wa mada wanazojifunza na mazoezi ya ziada," alisema. Silinde, aliwasihi kusimamia matumizi na utunzaji wa vitabu hivyo. "Ni wajibu wenu wasimamizi wa elimu kuhakikisha kwamba vitabu hivyo vinatumika kulingana na utaratibu unaokubalika," alisema.

Akizungumzia changamoto katika utayarishaji wa mitihani ya upimaji ya pamoja katika ngazi za halmashauri na mikoa kutokana na tofauti za ukamilishaji wa mada kati ya shule moja na nyingine au kati ya halmashauri moja na nyingine, alisema kalenda hiyo iwe dira mahsusi ya kupanga utaratibu wa kuandaa mitihani ya pamoja kama ujirani mwema wa shule na utimilifu.

"Ni matumaini yangu kuwa maofisa elimu wa mkoa kwa kushirikiana na maofisa elimu taaluma mtatumia kalenda hii wakati wa kuandaa mitihani hiyo ili kupata mitihani inayotokana na mada zilizofundishwa na kukamilishwa katika shule zote nchini," alisema.

Alisema kuwa kalenda hiyo itasaidia kupunguza uwezekano wa viongozi wa walimu kulazimishwa kukamilisha mada kabla ya muda uliopangwa.

"Kutokana na majadiliano yenu, imeonekana haja ya kuwa na uchambuzi wa kina wa mawanda ya kalenda hii kwa kuzingatia hali halisi na tofauti za maeneo yenu ya utekelezaji. Ninatumia fursa hii kuwaelekeza maofisa elimu wa mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha kuwa, mnafanya uchambuzi wa kina wakati wa utekelezaji ili muweze kubainisha changamoto na namna ya kuzishughulikia," alisema.

Aliwatoa hofu kuwa kalenda hiyo haitamwondolea mwalimu ubunifu wake wa ufundishaji kama alivyokuwa anafanya kabla ya kuanza kutumia.

Naibu Katibu Mkuu, TAMISEMI anayeshughulikia elimu, Gerald Mweli, alisema kalenda hiyo imetengenezwa ili kuleta mfanano kwenye utekelezaji wa mitaala nchini na kupima utekelezaji wa mitaala kwa walimu.

# Samia kufungua jengo la Jumuiya ya Wazazi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kufungua jengo la Jumuiya ya Wazazi lililoko jijini Dodoma lililogharimu zaidi ya Sh. milioni 230.

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Dk. Edmund Mndolwa, alitoa wito kwa wabunge wanaotokana na chama hicho kujitokeza kuchangia samani kwenye jengo hilo ili lianze kutumika.

Akizungumza jijini hapa jana baada ya kukabidhiwa jengo hilo lililojengwa na Jitegemee Trading Company Limited (JTCL) kwa kushirikiana na kitengo cha miliki, Dk. Mndolwa, alisema amemwomba Rais Samia kuja kuzindua jengi hilo na amekubali.

"Nilimdokeza mama Samia kuwa tutakabidhiwa jengo hili na nitakuomba mama uje utufungulie, amekubali sasa ni sisi kufuatilia makubaliano hayo. Nina hakika wenzetu wengine pia wa jumuiya ambao mejengo yao yapo tayari nadhani watataka pia mama awafungulie, lakini hiyo ni kwao. "Lakini mimi navuta kamba upande wangu ili tufungue mapema zaidi," alisema Dk. Mndolwa.

Alisema tayari wamekabidhiwa jengo hilo na kazi iliyopo ni kutafuta fedha kwa ajili ya ununuzi wa samani za ndani huku akiishukuru kamati ya utendaji kwa ushirikiano walioutoa na kusababisha kukamilika kwa jengo hilo. Mwenyekiti huyo alitoa wito kwa wabunge wa Jumuiya na wanaotokana na chama, walimu, wakuu wa jumuiya kujitokeza kwa wingi kuchangia samani ili Rais akija kuzindua kazi zianze rasmi ndani ya jengo.

"Jengo ni jengo lazima tukae kwenye viti na meza hivyo wabunge wa jumuiya na wengine watusaidie ili tuingie na kufanya kazi kwa ufanisi hata viongozi wengine wakija tutawapa ofisi wafanyie kazi maana hii ni jumuiya kongwe inayotegemewa na watu, hivyo lazima tuwe na jengo zuri," alisema.

Kwa upande wake, Katibu wa Jumuiya, Gilbert Kalima, alisema wabunge wa Jumuiya ya Wazazi wamekabidhi vifaa kwa ajili ya ofisi nne huku akitoa wito kwa viongozi wengine kutoa michango ukiwamo ushauri namna ya kupata samani hizo za ofisi.

Mwenyekiti wa Bodi ya Jitegemee, Martha Luleka, alisema kutokana na maboresho mazuri ya mradi huo kampuni inaamini chama kitawapa miradi mingine.

"Tunaamini mtatupa kazi nyingine maana huu ni mradi wa kwanza kuukamilisha tuna miradi mingine miwili ya jengo la vijana ambao umekamilika na wa jengo la wanawake ambalo ujenzi wake unaendelea na tutakabidhi muda wowote ukikamilika," alisema.

Awali, akisoma taarifa ya ukarabati wa jengo hilo, Meneja wa kampuni hiyo, Zainab Juma, alisema awali jengo hilo lilikuwa la ghorofa moja na sehemu ya juu isiyofunikwa lilihitaji ukarabati na maboresho makubwa.

Alibainisha ujenzi huo ulianza Machi mwaka jana na hadi sasa umetumia miezi 10 kukamilika.

Alisema katika mkataba wa awali gharama za ukarabati na maboresho mbalimbali zilikuwa Sh. milioni 216, lakini kulikuwa na ongezeko la kazi lililotokana na mahitaji ya mteja na kuongezeka na kufikia Sh. milioni 230.

Alisema jengo hilo lina vyumba vya ofisi 16, mapokezi moja, masijala ya siri moja, masijala ya wazi moja, ukumbi wa mkutano mmoja, sehemu ya kuandalia chai na vyoo 11.

"Tunakishukuru chama kwa ulezi wake bora wa jumuiya zake, lakini tunaishukuru Jumuiya ya Wazazi kwa ushirikiano mkubwa waliotuonyesha kuanzia mwanzo hadi mwisho wa ukarabati wa jengo hilo," alisema.

# TANESCO kuendelea kuunganisha umeme Sh. 27,000

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) limewahakikishia wananchi wa maeneo ya vijijini nchini kuwa wataendelea kuwaunganishia huduma ya umeme kwa gharama ya Sh. 27,000.

Meneja Mwandamizi wa Shirika hilo Kanda ya Kati, Mhandisi Frank Chambua, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati alipofanya ziara ya kutembelea Kijiji cha Kigwe, Wilaya ya Bahi.

Chambua alisema TANESCO itaendelea kuwaunganishia umeme wananchi wote nchini wa meneo ya vijijini kwa gharama hizo ili kunufaika na huduma hiyo.

"Naomba kuwahakikishia wananchi wa maeneo yote vijijini nchini kuwa TANESCO tunaendelea kuwaunganisha huduma ya umeme kwa bei ya Sh. 27,000 tu kupitia miradi inayotekelezwa na shirika letu meneo mbalimbali nchini," alisema Chambua.

Alisema lengo la ziara hiyo kwenye kijiji hicho ni kuwaelimisha na kuhamasisha wananchi wa maeneo ya vijijini kuunganisha huduma hiyo na itaendelea kuwa ile ile.

Alifafanua kuwa, serikali imefadhili miradi ya umeme kwenye maeneo ya vijijini na wananchi wanatakiwa kuendelea kulipia hizo zilizotajwa ikijumuisha ghrama za Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Kadhalika, Chambua alisema shirika hilo limeendelea na utaratibu huo wa kutoa elimu ili kuepusha wananchi kufanyiwa utapeli na watu wasio waaminifu.

Alitoa wito kwa wananchi wa mkoa huo kusaidia kulinda miundombinu ya umeme hasa kipindi hiki cha maandalizi ya msimu wa kilimo.

Aliwataka kuacha kuchoma moto mashamba kwa sababu umekuwa ukisababisha kuunguza nguzo za umeme zilizopita kwenye maeneo hayo.

Naye mkazi wa kijiji cha Kigwe, Nasia Samwel, alilishukuru shirika hilo kwa kuendelea kuwatoza kiasi hicho cha fedha ambacho kitawasaidia kumudu gharama hizo.

Nasia alisema kuunganishwa kwa umeme kwenye kijiji chao itawasaidia vijana kujiajiri kwenye sekta ya uchomelejia na kuanzisha saluni za kike na kiume.

Pia, alisema kuwapo kwa umeme kwenye eneo hilo kutasaidia kuwavutia wawekezaji watakaojenga viwanda ambavyo vitatoa ajira kwa wazawa wa hapo.

Kwa upande wake, Kaimu Meneja wa TANESCO Wilaya ya Bahi, Hassan Hassan, alisema wanaendelea kuwaunganishia huduma hiyo wateja wote wa maeneo ya vijijini waliolipia na wanaoendelea kulipa.

Alisema kwa siku hiyo jumla ya wateja wapya 16 wa kijiji hicho walifanikiwa kuunganishiwa na wengine wamehamasika kulipia baada ya kuona wenzao wameunganishiwa.

Aidha, alisema Mkoa wa Dodoma serikali imewekeza Sh. bilioni 195.5 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kuunganisha umeme.

Aliongeza kuwa fedha hizo zimesaidia kutoa huduma hiyo kwa jumla ya vijiji 581 na mpaka sasa vijiji 422 vimefikiwa na huduma hiyo na vilivyobaki ni 159 na wakandarasi wanaendelea na kazi ya kuunganisha.



## H'shauri zashauriwa kutenga bajeti shule mchepuo Kiingereza

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI zote za Mkoa wa Mbeya, zimeagizwa kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa shule za msingi za mchepuo wa Kiingereza ili kuwaandaa vizuri wanafunzi kwenye misingi ya lugha ya Kiingereza pamoja na kuongeza vyanzo vya mapato.

Agizo hilo lilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alipofanya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa kwenye shule za sekondari na msingi katika Jiji la Mbeya.

Aliwataka watendaji wa halmashauri hizo kwenda kujifunza ujenzi na uendeshaji wa shule hizo katika Jiji la Mbeya ambalo tayari lina shule tano za aina hiyo na inaendelea na mipango ya ujenzi wa shule zingine za aina hiyo.

Alisema baadhi ya wazazi wanapenda kuwapeleka watoto wao kwenye shule za aina hiyo, lakini kutokana na kutokuwapo jirani, wanalazimika kuwapeleka maeneo ya mbali hali ambayo alisema huwa sio nzuri.

Alisema halmashauri hizo zinatakiwa kuchangamkia fursa hiyo kabla wawekezaji binafsi hawajaziba nafasi huku akiagiza zoezi hilo kuwa la lazima.

"Na hii ni lazima kwa halmashauri zote, Katibu Tawala waandikie barua wakurugenzi wote kwamba ni lazima watenge bajeti ya ujenzi wa shule hizi kwenye maeneo yao, kukosekana kwa shule hizi maeneo mengine kunasababisha msongamano wa watoto kwenye shule zilizoko hapa mjini," alisema Homera.

Hata hivyo, alipongeza uongozi wa Jiji la Mbeya kwa ujenzi na usimamizi wa shule hizo kuwa zinaendelea kutokana na ushirikiano wa uendeshaji kati ya watumishi wa jiji na madiwani.

# Kampuni zinazonunua tumbaku zajiondoa

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

UZALISHAJI wa tumbaku katika Mkoa wa Kitumbaku wa Chunya, unatarajiwa kushuka kutoka kilogramu milioni 10.8 za msimu uliopita mpaka milioni 10.3 msimu huu kutokana na baadhi ya kampuni za ununuzi wa zao hilo kujiondoa.

Kipato cha wakulima kinachotokana na zao hilo kinatarajiwa kushuka kutokana na kupungua kwa kiwango cha uzalishaji hali ambayo inadaiwa kuwa itaathiri uendeshaji wa kilimo hicho pamoja na uchumi wa wakulima.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wa Tumbaku (CHUTCU), Sebastian Mogella, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano mkuu wa kawaida wa wanachama wa chama hicho uliolenga kujadili mambo mbalimbali yakiwamo kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema kwa sasa mkoa huo umebakiwa na kampuni moja pekee ya ununuzi, Premium Active Tanzania LTD (PATL), ambayo imeingia mkataba wa ununuzi wa na vyama vya msingi 22 vya mkoa huo kununua tumbaku yao.

Alisema chama kikuu kimeshindwa kupata wanunuzi wengine wa zao hilo kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo baadhi ya kampuni kugoma zikiogopa kuongeza gharama za uwekezaji kutokana na jiografia zinakofanya kazi kwa sasa.

Alisema baadhi ya kampuni zilizoombwa kwenda kununua tumbaku hiyo ni Allience One na JTI ambayo inanunua zao hilo mkoa jirani wa Tabora, lakini zilikataa na baadhi ya vyama kukosa wanunuzi baada ya kampuni zilizokuwa zinanunua kujiondoa.

"Kulikuwa na hatari ya baadhi ya wanachama kutoshiriki kilimo cha tumbaku msimu huu wa 2021/2022, sasa tuliamua kufanya mazungumzo na wenzetu PATL ili kugawana uzalishaji kwenye vyama vyote na wamekubali," alisema Mongella.

Vilevile, alisema kutokana na kampuni zingine kujitoa, Kampuni ya PATL imeongeza kiwango cha ununuzi wa tumbaku kutoka kilogramu milioni 9.45 msimu uliopita mpaka kilogramu milioni 10.3 ambazo ndizo wakulima wanatarajiwa kuzalisha.

Ofisa Kilimo wa Wilaya ya Chunya, Cathbert Mwinuka, aliwataka wakulima wa tumbaku kulima na mazao mengine ili kuepuka kuathirika kiuchumi kutokana na mabadiliko ya tabianchi yanayoikumba nchi kwa sasa ambayo yanaweza yakaathiri kilimo hicho.

Alisema kwa sasa wakulima wanasisitizwa kupanda mazao yanayokomaa kwa muda mfupi na yanayostahimili ukame ili kuepuka madhara ya hali hiyo ya mgawanyiko mbaya wa mvua nchini.

Alisema yapo mazao ambayo wakulima wanashauriwa kuzalisha ikiwamo alizeti, viazi vitamu na mihogo na kuwataka wakulima hao kuyalima ili yawasaidie endapo kutatokea madhara kwenye tumbaku.

"Wataalamu wa hali ya hewa wameshatoa taarifa kuwa mwaka huu kutakua na mgawanyiko mbaya wa mvua, kuna maeneo inanyesha na maeneo mengine hainyeshi, sasa haya mabadiliko ambayo hatukuyatarajia yanaweza yakatuathiri, hivyo jitahidini kulima mazao sambamba," alisema Mwinuka.

Vilevile, aliwataka wakulima hao kufuata taratibu za kilimo cha tumbaku wanazoelekezwa na wataalamu ikiwa ni pamoja na kuepuka kuchanganya madaraja wakati wa kufunga mitumba.

Kwa upande wake, Mrajisi Msaidizi wa vyama vya ushirika Mkoa wa Mbeya, Richard Zengo, aliwataka viongozi wa vyama vya ushirika katika mkoa huo kufuata taratibu za usimamizi wa vyama hivyo kama walivyoahidi kwenye viapo vyao.



Baadhi ya wahitimu wa kidato cha nne katika Shule ya St Francus ya jijini Mbeya wakimpongeza mwenzao, Bhutoi Nkangaza (mwenye gauni la kitenge) ambaye ameshika nafasi ya pili kitaifa walipokutana shuleni hapo mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Maduka 8 yafungiwa kwa kuuza mbegu feki

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu nchini (TOSCI), imeyafungia maduka nane kufanya biashara ya mbegu katika mikoa ya Mbeya na Songwe baada ya kubainika kuwa yanauza mbegu feki na zingine zimeingizwa kutoka nje ya nchi bila kutibitishwa ubora wake.

Aidha, baadhi ya maduka hayo yamefungiwa kutokana na kufanya biashara ya mbegu bila kusajiliwa na taasisi hiyo huku wafanyabiashara hao wakiwa hawana mafunzo ya uuzaji wa mbegu kwa mujibu wa sheria.

Taasisi hiyo iliyafungia maduka hayo mwishoni mwa wiki baada ya kufanya ukaguzi wa kushtukiza kwenye maduka mbalimbali kwa ajili ya kuhakiki aina ya mbegu ambazo wakulima wa mikoa hiyo wanauziwa katika kipindi hiki cha kilimo.

Maofisa wa TOSCI wa Kanda ya Nyanda za Juu kwa kushirikiana na taasisi zingine ndiyo waliofanya ukaguzi huo na walisema katika kipindi hiki ambacho wakulima wanakimbizana na msimu wa kilimo, wafanyabiashara wengi wanakuwa wadanganyifu.

Ofisa Mfawidhi wa TOSCI Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Peter Nassari, alisema katika operesheni hiyo walikagua maduka zaidi ya 200 kwenye mikoa hiyo na inaendelea katika mikoa yote ya ukanda huo.

Alisema endapo wafanyabiashara hao wataendelea kuwauzia wakulima mbegu hizo, kuna hatari ya uzalishaji kushuka kutokana na baadhi ya mbegu hizo kutoota na hata zinazoota uzaaji wake ni tofauti na matarajio ya wakulima.

Vilevile, alisema uingizaji wa mbegu kutoka nje ya nchi ambazo hazijathibitishwa ubora wake unaweza ukasababisha kusambaa kwa magonjwa ya mazao na hivyo kusababisha hasara kwa wakulima na kwa taifa.

"Nawaomba wakulima wajitahidi kuzichunguza mbegu kabla hawajazinunua, waangalie kwanza kama zina nembo ya TOSCI na wahakikishe wanapewa risiti ili iwe rahisi kufuatilia endapo kutatokea tatizo," alisema Nassari.

Baadhi ya wafanyabiashara wa mbegu walisema wanashindwa kutofautisha mbegu feki na nzuri kutokana na kutopatiwa mafunzo ya mara kwa mara hali ambayo walisema hata wao wanaingia hasara baada ya kuzuiwa kuziuza mbegu ambazo wananunua kwa bei kubwa.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, William Mbua, alisema maduka ya kuuza pembejeo za kilimo yanafungiwa kila siku, lakini mafunzo ya kuzitambua mbegu yanatolewa mara chache hali ambayo inawafanya baadhi ya wafanyabiashara kuuza mbegu bila kuzijua ubora wake.

Alisema mbali na maduka mapya kufunguliwa na wakulima, lakini hata mbegu mpya zinazalishwa kila mwaka na kuiomba serikali kuwekeza zaidi kwenye mafunzo ya wauzaji wa pembejeo za kilimo.

"Ni kweli baadhi ya wafanyabiashara wanakuwa sio waaminifu kwa sababu hiyo ni tabia ya binadamu, lakini baadhi huwa wanauza mbegu feki kwa kutokujua kutokana na kutopata mafunzo, hivyo tunaomba TOSCI wajitahidi kutoa elimu ya mara kwa mara," alisema Mbua.

Nao wakulima walisema mbegu feki zimekuwa zikiathiri sekta ya kilimo kwa kuwaongezea gharama za uzalishaji wakidai kuwa baadhi ya mbegu huwa hazioti na kulazimika kupanda upya.

Mmoja wa wakulima hao, Winfrida Jaston, ambaye analima nyanya alisema mbegu feki huwa zinakuwa na picha ambayo haiendani na kilichomo ndani kwa maelezo kuwa vifungashio vinakuwa na maelezo mazuri kuliko uhalisia.

Alisema mbegu hizo zinakuwa na picha na maelezo ambayo yanaonyesha kuwa kipato chake ni kikubwa, lakini wakilima wanapata matokeo tofauti.



# Taasisi ya Marekani yasaidia vifaa tiba Wizara ya Afya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TAASISI ya Helping Hand kutoka Marekani kwa kushirikiana na Taasisi ya Muzdalifa Zanzibar, imeikabidhi Wizara ya Afya Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto Zanzibar, msaada wa vifaa tiba vyenye thamani ya Dola za Marekani 114,521.72. Makabidhiano hayo yalifanyika jana Wizara ya Afya Mnazi Mmoja na kumkabidhiwa Waziri wa wizara hiyo, Nassor Ahmed Mazrui.

Akizungumza baada ya makabidhiano hayo Waziri Mazrui alisema msaada huo utawasaidia wataalamu wa afya kuendelea kutoa huduma bora kwa jamii.

Alisema bila afya bora maendeleo hayatopatikana hivyo serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kutoa huduma bure za afya kwa wananchi.

Alisema kuwa, lengo la msaada huo ni kuwasaidia wananchi na kuihakikishia taasisi hiyo kuwa vifaa hivyo vinatumika ipasavyo na kuwafikia walengwa.

"Nataka niwaambie watendaji hivi vifaa mvitunze, lakini ni marufuku kuviuza au kuvitumia kinyume na utaratibu," alisisitiza Mazrui. Aliahidi kuendeleza ushirikiano wa karibu baina ya Wizara ya Afya na Taasisi hiyo ili lengo la kuboresha sekta ya afya kufikiwa nchini.

Naye Mshauri Msaidizi wa Taasisi ya Helping Hand, Irfan Khurshid, alisema msaada huo ni miongoni mwa jitihada za kuisaidia sekta ya afya Zanzibar kutoa huduma bora kwa jamii.

Alisema taasisi hiyo ina mpango wa kuendelea kutoa misaada mbalimbali ya sekta ya afya ili wananchi wa Unguja na Pemba wanufaike.



Mkurugenzi wa Wakala wa Mtandao Zanzibar, Said Seif Said (kushoto), akimkabidhi hati ya makubaliano ya ushirikiano wa kazi Mkurugenzi wa World Mobile, Rajabu Thabit Rajab, Mjini Zanzibar mwishoni mwa wiki. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## World Mobile, E Government zaingia makubaliano

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKALA wa mtandao wa simu wa kampuni ya simu duniani (World Mobile), imetiliana saini makubaliano ya utendaji kazi na wakala wa mtandao Zanzibar (E Government) ili kutatua changamoto za kimifumo kwenye uchumi wa bluu na huduma za intaneti katika maeneo ya wazi.

Utiaji saini wa makubaliano hayo umefanyika jana katika ofisi za E Government Mazizini na kusainiwa na Mkurugenzi wa Wakala wa Mtandao Zanzibar, Said Seif Said na kwa upande wa kampuni ya World Mobile umesainiwa na Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Rajabu Thabit Rajab.

Akizungumza baada ya utiaji saini wa makubaliano hayo Mkurugenzi wa World Mobile Rajab aliyataja maeneo hayo ya wazi ambayo yatakuwa na huduma za mawasiliano ya intaneti ni uwanja wa ndege, bandarini, hospitali, sokoni na maeneo mengine ya serikali ili kurahisisha upatikanaji wa mawasiliano.

Alisema ushirikiano huo utaanza kuunganisha huduma ya teknolojia ya mawasiliano ya intaneti katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Abeid Amani Karume.

"Hii ni hatua ya kwanza ya ushirikiano kabambe na mpango wa miaka mitano ambao utakuza kwa kiasi kikubwa pato la taifa la Zanzibar," alisema.

Alisema kampuni hiyo pia imepewa fursa ya kuzifikia shule zote za serikali Zanzibar na taasisi za elimu kwa ajili ya kufunga mtandao wa intaneti na shule hizo zitapata mgawo wa mapato kutoka kwa watumiaji wa teknolojia hiyo.

Naye Mkurugenzi wa Wakala wa Mtandao, Said Seif, alisema ni faraja kushirikiana katika kukuza teknolojia ili kupata huduma muhimu za mtandao.

Alisema makubaliano hayo yatasaidia kukuza uchumi wa bluu kupitia teknolojia hiyo.

"Itatupa nafasi ya haraka ya kufikia maendeleo ya dunia katika matumizi ya teknolojia inayoenda kwa kasi duniani," alisema.

# 'Jihadharini kutoa zawadi ya mitungi yenye gesi ndani'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

LICHA ya bidhaa ya gesi ya kupikia ni rafiki wa mazingira na salama katika matumizi kama bidhaa zingine, lakini kuna tahadhari zinapaswa kuchukuliwa ili kuepusha maafa.

Hayo yalielezwa na Ofisa Uhusiano wa Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Mbaraka Hassan, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu utoaji wa zawadi wa majiko ya gesi yakiwa na mitungi ya gesi ndani katika shughuli za harusi baada ya kusambaa kwa video za utoaji wa zawadi za nishati hiyo mbadala katika moja ya harusi iliyofanyika mwisho wa mwaka jana mjini hapa.

Alisema kuwa haikubaliki kuingiza mitungi ya gesi katika ukumbi kwenye sherehe na kuigawa kama mfano wa njugu jambo ambalo ni hatari kwa usalama wa wananchi.

Alisema hawakatazi utoaji wa zawadi hiyo katika sherehe bali kuwe na utaratibu wa kiusalama wakati wa ugawaji wa mitungi ya gesi.

Alisema waligundua utoaji wa majiko ya gesi wakati kitendo hicho kilishafanyika, lakini waliwafuata watoaji na kuwapa utaratibu unaotakiwa kufuatwa.

Alisema ni hatari katika mikusanyiko ya watu kutoa mitungi ya gesi ndani ya ukumbi kwa sababu unahatarisha usalama wa wananchi.

"Hata katika vyombo vya usafiri tunatumia vyombo vinavyotumia nishati ya mafuta ya petroli ambayo nayo ni hatari, lakini kuna tahadhari zinapaswa kuchukuliwa," alisema Hassan.

Sherehe ya harusi hiyo iliyotolewa zawadi kwa waalikwa majiko ya gesi yakiwa na gesi ilizua gumzo katika mitandao ya kijamii.

Baadhi ya wananchi waliohudhuria sherehe hiyo ambao hawakutaka kutajwa majina yao walisema sherehe hiyo ilifana na ni neema kwao kwa kupatiwa nishati hiyo mbadala ya kupikia.

"Nilikuwa sina jiko la gesi napikia mkaa, lakini kutunukiwa zawadi hii ya jiko la gesi imenirahisishia kumaliza kupika mapema nyumbani kwangu," alisema mmoja ya waalikwa wa shughuli hiyo.

Alisema kuwa kila mmoja aliyealikwa katika shughuli hiyo alipatiwa jiko la gesi la ujazo wa kilo sita likiwa na gesi lenye thamani ya Sh. 50,000.

"Sherehe ile ya harusi ilikuwa ya aina yake maana haijawahi kutokea kwa Zanzibar kugaiwa majiko ya gesi," alisema.

Hivi karibuni Mhandisi wa migodi kutoka Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Charles Mawala, wakati akitoa mada ya matumizi ya mkaa mbadala katika kongamano la utunzaji wa mazingira lililofanyika viwanja vya Maisara mjini Zanzibar, alisema hekta 470,000 za ardhi zenye misitu zinaathiriwa nchini Tanzania kwa mwaka kutokana na ukataji miti kwa ajili ya nishati ya mkaa.

Alisema hali hiyo inaathiri mazingira kwa sababu miti husaidia kuvuta hewa chafu kama carbon dioxide inayotokana na shughuli zote za maendeleo.

"Gesi hizi huchangia pakubwa kwenye uharibifu wa tabaka ozone na kuleta majanga kama ukame," alisema.

Alisema kutokana na ongezeko hilo la ukataji wa miti kila mwaka, Shirika la Madini la Taifa liko mbioni kuanza uzalishaji wa mkaa mbadala (Rafiki briquettes) ambao ni muafaka kwa matumizi ya kijamii kama kupikia.

Alisema mkaa huo ni suluhisho kwa tatizo la kimazingira la hatari ya kutokea jangwa inayosababishwa na ukataji ovyo wa misitu kwa ajili ya nishati ya kuni na mkaa wa kuchoma.

# RPC awatunuku askari 15 uwajibikaji mzuri

**Na Said Hamdani, LINDI**

JESHI la Polisi mkoani Lindi limewatunuku vyeti na zawadi askari 15 kutambua na kuthamini michango yao wawapo vituo vyao vya kazi.

Askari hao kutoka vituo mbalimbali, wamekabidhiwa vyeti hivyo na Kamanda wa Polisi mkoani humo, ACP Mtatiro Kitinkwi, katika hafla iliyofanyika mjini hapa.

Akizungumza wakati wa kukabidhi zawadi kwa wahusika, aliwataka wengine kuongeza uwajibikaji na nidhamu ndani na nje ya maeneo yao ya kazi, kwa kujiepusha kushiriki vitendo vya kuomba na kupokea rushwa.

"Zawadi hizi mlizokabidhiwa ni sehemu ya kuthamini na kutambua michango yenu na iwe chachu kwa askari wengine ambao hamjapata," alisema Kitinkwi.

Alisema vitendo viovu mara nyingi vinachafua na kupoteza sifa na nia njema kwa jeshi hilo ambalo miongoni mwa majukumu yake ni kuhakikisha raia na mali zao wanakuwa salama wakati wote.

Vile vile, alisema askari atakayebainika kujihusisha na vitendo vinavyochafua jeshi hilo, ikiwamo kuomba na kupokea rushwa, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake ikiwamo kupoteza ajira na kufikishwa mahakamani.

Baadhi ya askari waliokabidhiwa vyeti na zawadi zingine ambao hata hivyo, majina yao hawakupenda kutajwa kwenye vyombo vya habari walisema zawadi walizopewa zimewaongezea morali wa uwajibikaji kazini, huku wengine wasiobahatika wakisema imeamsha mori na watahakikisha na wao wanafanya vyema.

Kwa zaidi ya miaka 20 utaratibu wa kuzawadia askari wanaofanya vizuri ndani ya Mkoa wa Lindi kwa muda mrefu ulikuwa umesahaulika, Kamanda ACP Kitinkwi ameanza kuurejesha upya.




Meneja Mauzo wa Tigo Ubungo, Sekirito Karia (watatu kushoto), akikabidhi zawadi ya pikipiki kwa mkazi wa Mapinga Bagamoyo, Aisha Bakari Hill, baada ya kuibuka mshindi wa wiki ya saba ya promosheni ya Wagiftishe Gift Juu ya Gift, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shule yataja siri wanafunzi kufanya vizuri

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

MIKAKATI mitatu iliyowekwa na uongozi wa Shule ya Sekondari St. Mathew's iliyoko Wilaya ya Mkuranga, mkoani Pwani, imezaa matunda baada ya wanafunzi wote waliomaliza kidato cha nne mwaka jana kufaulu mitihani yao ya taifa.

Mikakati hiyo iliyowekwa kwa wanafunzi ni elimu, usalama na malezi.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa shule hiyo, Peter Mutembei, baada ya Katibu Mkuu Baraza la Mitihani kutangaza matokeo ya Kidato cha Nne.

"Shule tulijiwekea mikakati mitatu kwa wanafunzi wetu, ambapo mikakati hiyo imezaa matunda na kufanikisha wote waliomaliza mitihani yao mwaka jana kufaulu kwa kishindo," alisema.

Aliongeza kuwa wanafunzi waliofanya mitihani yao mwaka jana walikuwa wahitimu 85 na 30 wakipata daraja la kwanza, 45 daraja la pili na 15 daraja la tatu na hakuna daraja la nne wala daraja la mwisho.

"Ufaulu huo unaifanya shule kuwa miongoni mwa zilizoongoza katika ufaulu wa matokeo hayo kuanzia ngazi ya wilaya, mkoa na taifa," alisema.

Alisema matokeo hayo yanafanya wanafunzi wote waliofanya mtihani St. Matthew's kuwa miongoni mwa waliopata ufaulu wa juu kitaifa kwa daraja la kwanza mpaka la tatu ikiwa ni asilimia 35.84 ya wanafunzi wote waliofanya mtihani wa taifa kidato cha nne mwaka 2021.

Pia aliwapongeza walimu, wazazi na wanafunzi kwa kujituma, kufanya kazi kwa bidii, kuwafundisha vizuri wanafunzi wao na kufanikiwa kupata ufaulu mzuri.

Alisema mkakati huo, ulisaidia wanafunzi wote waliomaliza elimu ya msingi mwaka jana katika shule hiyo kupata alama 'A' katika masomo yao, kiwilaya shule hiyo ilishika nafasi ya kwanza.

## Mil. 187/- kutolewa kwa wajasiriamali

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

HALMASHAURI ya Ushetu, wilayani Kahama mkoani Shinyanga, imetenga Sh. milioni 187 kwa ajili ya kutoa mikopo isiyo na riba katika makundi maalumu ya vijana, kinamama na watu wenye ulemavu kutoka kata 20 za halmashauri hiyo.

Fedha hizo zimetengwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 na zinatokana na mapato ya ndani ya halmashauri kutoka katika vyanzo vya mazao ya kibiashara ikiwamo tumbaku, pamba, mahindi na madini yanayochimbwa Kata ya Mwabomba.

Hayo yalibainishwa jana na Diwani wa Kata ya Nyamilangono, Robert Mihayo, wakati akizungumza na gazeti hili kuhusu usimamiaji wa vikundi vya wajasiriamali kupata mikopo ya asilimia 10 kutoka halmashauri hiyo.

Alisema, kwa mwaka huu wa fedha halmashauri hiyo imetoa mikopo kwenye Kata ya Nyamilangano yenye thamani ya Sh. milioni 36.3 kwa vikundi vitatu vya Tujipange kinamama, waendesha bodaboda na kikundi cha mtu mmoja mwenye ulemavu.

Aidha, alisema kati ya fedha hizo Sh. milioni 28.8 zimetumika kununua pikipiki 12 na kuzigawa katika kikundi cha bodaboda Nyamilangno, Shilingi milioni saba kwa kikundi cha Tujitengemee kinamama ambazo zitatumika kunenepesha mifugo na ufunguzi wa bucha ya nyama.

Pia Sh. 500,000 zimetolewa kwa kikundi cha mtu mmoja wenye ulemavu wa viungo ili kuinua mtaji na kuondokana na adha ya kuwa tengemezi kwenye jamii na familia hasa kupitapita mitaani na kwenye makazi yao watu kuomba msaada.

"Tumewawezesha vijana 12 pikipiki zenye thamani ya Sh. milioni 28.8 fedha kutoka asilimia 10 ya mapato yetu ya halmashauri, kila moja imegharimua Sh. milioni 2.4 na kila mwezi kila mmoja atarejesha Sh. 200,000 na mwishoni mwa mwaka huu watamaliza deni hilo," alisema Mihayo.

Mmoja wa wanufaika wa mikopo wa pikipiki, Charles John, alisema kabla ya kupewa pikipiki hiyo alikuwa anajishughulika na kilimo cha pamba na fedha alizokuwa akizipata alikuwa akihifadhi kwa ajili ya kununua pikipiki na kuendesha maisha.

HABARI KIMATAIFA

# Tahadhari kutokea tsunami yatolewa

**Nuku'alofa,** TONGA

JAPAN na Marekani zimewataka watu wanaoishi kwenye mwambao wa bahari ya Pacific, kuelekea sehemu za miinuko, kutokana na kitisho cha tsunami baada mlipuko wa volkano ya chini ya bahari karibu na kisiwa cha Tonga.

Tonga ni nchi ya visiwani ya Polynesia katika Pacific ya Kusini yenye wakazi 102,321. Eneo lake lina visiwa 169 Kusini kwa Fiji na Samoa na Kaskazini mwa New Zealand.

Picha za satelaiti zimeonyesha mlipuko wa volkano hiyo ya Hunga Tonga-Hunga Ha'apai, ambao umerusha angani moshi na majivu katika umbo la uyoga mkubwa na kusababisha tetemeko katika eneo la bahari ya Pacific linalokizunguka kisiwa cha Tonga.

Taarifa za Taasisi ya Hali ya Hewa Australia, zilisema mawimbi yenye kimo cha mita 1.2 yalishuhudiwa katika mji mkuu wa Tonga wa Nuku'alofa.

**Lilikuwa tetemeko kubwa sana lililoitikisa ardhi. Kaka yangu alidhani ni mabomu yaliyokuwa yakilipuliwa karibu na nyumba yetu.**

Japan pia iliripoti mawimbi yaliyotokana na tsunami hiyo yamefika kwenye pwani yake, yakiwa na kimo cha hadi mita tatu.

Hali hiyo ilisababisha taharuki na watu wa kisiwa kidogo cha Tonga walionekana wakikimbia mbio kuhamia kwenye maeneo ya vilima.

Mmoja wao, Mere Taufa, alisema wakati volkano ilipolipuka alikuwa nyumbani akijiandaa kwa mlo wa mchana na alishtushwa na mawimbi ya bahari yaliyoanza kuivamia nyumba yake.

"Lilikuwa tetemeko kubwa sana lililoitikisa ardhi. Kaka yangu alidhani ni mabomu yaliyokuwa yakilipuliwa karibu na nyumba yetu," alisema Taufa akizungumza na tovuti ya Stuff News.

Mkazi huyo alisema nyumba yao ilifurika maji katika muda wa dakika chache na kuongeza, aliuona ukuta wa nyumba ya jirani yake ukiporomoka.

"Bila kukawia tulijua kuwa ni tsunami imetokea, kwa kiwango cha maji yaliyoivamia nyumba yetu. Ungeweza kuwasikia watu wakipiga mayowe kila mahali, wakikimbilia maeneo salama, kila mmoja akitafuta sehemu iliyoinuka."

Mlipuko huo wa volkano ya chini ya bahari, ulidumu kwa takribani dakika nane na umekuja muda mfupi baada ya kutolewa kwa tahadhari ya tsunami nyingine.

Kulingana na duru kutoka mji wa Suva, mlipuko huo ulisikika kama mungurumo wa radi katika kisiwa cha Fiji kilichoko umbali wa kilomita 800 kutoka kitovu chake na mawimbi makubwa yaliipiga pwani ya kisiwa hicho.

Miito ya tahadhari imetolewa pia New Zealand, American Samoa, Vanuatu, Chile na Australia.

Onyo la tsunami lilitolewa pia kwa watu waishio pwani ya Magharibi ya Marekani, kuanzia California hadi Alaska.

Katika tangazo lake, kitengo cha Marekani cha tahadhari dhidi ya Tsunami, kimewaonya watu wanaoishi katika maeneo yanayokabiliwa na kitisho, kikisema 'tsunami inakuja, kikisema mawimbi ya mwanzo hayaonekani makubwa sana.

"Ondoka kwenye mwambao mhamie kwenye miinuko."

Canada pia imetoa angalizo kama hilo kwa watu wa mkoa wa British Columbia, ikiwaasa kuepuka kwenda ufukweni. **DW**

## Boris Johnson hatihati kujiuzulu kwa kukiuka masharti corona

**London,** UINGEREZA

VYOMBO vya habari Uingereza, vinaendelea kuzungumzia kuhusu uwezekano wa mtu mwingine kuchukuwa nafasi ya Waziri Mkuu wa sasa Boris Johnson, baada ya mvutano uliozuka kufuatia kukiuka kwake kwa sheria za kudhibiti ugonjwa wa Covid-19.

Katika vyombo vya habari vya Uingereza, tayari kuna uvumi kuhusu enzi ya baada ya Boris.

Vyombo vya habari Uingereza, vimekuwa vikizungumza juu ya Boris Johnson kupoteza imani yake kwa muda sasa.

Swali sasa ni lini na vipi atafukuzwa kazi, kwa kura ya kutokuwa na imani naye, kwa mfano, kujiuzulu kwake kwa moja kwa moja, kulingana na mwandishi wetu wa London, Sidonie Gaucher.

Hata kutoka kwenye chama chake, baadhi ya wabunge na maseneta nao wanamtaka aondoke serikalini.

Kwa hiyo Boris Johnson, anaweza kulazimishwa kujiuzulu, shinikizo kutoka kwa chama chake na kutoka kwa serikali ikiwa kura za kutosha zitakusanywa kati ya walio wengi.

Kwa mujibu wa Sophie Loussouarn, daktari aliyebobea katika historia ya kisiasa ya Uingereza; kujiuzulu huku sio sawa, kwa sababu katikati ya mgogoro wa kiafya, haitakuwa sahihi kufanyika kwa uchaguzi kwa uongozi wa Chama cha Conservative.

Majina ya watu kadhaa wanaoshukiwa kuchukuwa mikoba ya Boris Johnson yameanza kutajwa.

Kwanza, kuna Rishi Sunak, Chancellor of the Exchequer, yaani Waziri mwenye dhamana ya Fedha na Hazina? ambaye aliteuliwa kwenye nafasi hiyo Februari 13, mwaka jana. **RFI**



Gati imepasuka eneo la Marina huko Tutukaka, nchini New Zealand, jana, baada ya mawimbi makubwa ya bahari. Volcano ya chini ya bahari ililipuka karibu na Tonga na kusababisha tsunami huku watu wakikimbilia sehemu zenye miinuko kujinusuru. **PICHA: AP**

## Seneta Haiti ahusishwa na mauaji Rais Jovenal Moise

**Port-au-Prince,** HAITI

POLISI imesema seneta wa zamani wa Haiti, ambaye ni mshukiwa mkuu katika mauaji ya aliyekuwa Rais Jovenal Moise, ametiwa mbaroni akiwa nchini Jamaica.

Msemaji wa Jeshi la Polisi, Gary Desrosiers, ameliambia shirika la habari la Associated Press kwamba, John Joel Joseph, yuko chini ya ulinzi katika mahabusu.

Hakuna taarifa zaidi zilizopatikana kuhusu kukamatwa kwake.

Wakati hayo yakijiri, Kamanda wa Jeshi la Polisi Jamaica, Stephanne Lindsay, aliliambia shirika la habari Associated Press kwamba, watu wengine wamekamatwa pamoja na Joseph na maofisa wanajaribu kubaini ikiwa ni jamaa wa familia.

Kamanda huyo alithibitisha watu hao walikamatwa Jumamosi alfajiri, hakutoa taarifa zaidi.

Watu waliokuwa na silaha waliyavamia makazi binafsi ya Rais Moise, katika vilima vya mji wa Port-au-Prince, Julai 7, mwaka jana na kumuua kwa risasi. **DW**

# SIMBA, YANGA, GEITA GOLD ZATIKISA USAJILI

Na Adam Fungamwango

WAKATI dirisha dogo la usajili wa Ligi Kuu Tanzania Bara likifungwa juzi saa sita usiku, Klabu za Simba, Yanga na Geita Gold zimeonekana kutikisa kwenye dirisha dogo la usajili kutokana na wachezaji waliowasajili.

Simba haijafanya usajili mkubwa sana kipindi hiki, lakini imetikisa kutokana na kumrejesha mchezaji kipenzi cha wanachama na mashabiki wa timu hiyo, Clatous Chama aliyetimkia RS Berkane Morocco mwanzoni mwa msimu huu, huku watani zao wa jadi pamoja na kusajili wachezaji wazuri, lakini imekuwa moja ya timu iliyosajili wachezaji wengi kipindi hiki.

**Geita Gold ndiyo timu iliyoongoza kwa kusajili wachezaji wengi zaidi, kwani kabla ya dirisha dogo kufungwa, tayari ilikuwa imeshasajili wachezaji saba.**

Chama aliwasili Ijumaa jioni akitokea Zambia kuitumikia tena timu yake ya zamani na amesafiri na timu hiyo jijini Mbeya kwenye mechi ya leo dhidi ya Mbeya City.

Kwa upande wa Yanga, imefanya usajili wa maana kwa kuwasajili Denis Nkane kutoka Biashara United, Crispin Ngushi wa Mbeya Kwanza, Salum Aboubakar kutoka Azam FC, Aboutwalib Mshery (Mtibwa Sugar) na Ibrahim Bacca kutoka KMKM.

Geita Gold imewasajili William Gallas, ambaye chimbuko lake ni kikosi cha pili cha Simba na kupandishwa kikosi cha kwanza 2012, na straika kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Erick Yema.

Wengine ni Adeiyum Suleiman na Ditam Nchimbi kutoka Yanga, pia wapo Juma Nyosso na Kelvin Yondani pamoja na Aron kalambo.

Azam FC, imefanya usajili wa mchezaji Ibrahim Ajibu kutoka Simba, 'Messi wa Tanga' Issa Abushehe akisajiliwa na Dodoma Jiji kutokea Coastal Union, Prisons ikimsajili Mudathir Said akisajiliwa na Hamad Rajab 'Majimengi' akisajiliwa na Ruvu Shooting na wote hao wanatoka Coastal Union.

MAANDALIZI...



Usajili mpya wa dirisha dogo Simba, kiungo Clatous Chama (wa tatu kulia), akiwa gym jijini Mbeya baada ya timu hiyo kuwasili juzi tayari kwa mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Mbeya City utakaopigwa leo katika Uwanja wa Sokoine, akiwa sambamba na wachezaji wenzake wa timu hiyo viungo, Jonas Mkude (kulia) na Rally Bwalya. **PICHA: SIMBA**

# Biashara, Kagera zaweka rekodi ya mabao

Na Adam Fungamwango

SARE ya mabao 3-3 iliyopatikana juzi kwenye Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara kati ya wenyeji Biashara United dhidi ya Kagera Sugar, imezifanya timu hizo kuweka rekodi ya mabao mengi zaidi kufungwa kwa mara ya kwanza kwenye mechi za Ligi Kuu msimu huu.

Jumla ya mabao sita yamefungwa kwenye mechi moja na kuifanya kuwa mechi iliyozaa mabao mengi katika ligi hiyo mpaka sasa msimu huu.

Ni mechi iliyokuwa na ushindani mkubwa, ubabe, piga nikupige na funga nikufunge, wageni wakitangulia kwa mabao mawili, lakini wenyeji walisawazisha yote na kuweka kimyani la tatu kwa muda mfupi tu, lakini wakati kila mmoja akijua Biashara United ingeibuka na ushindi, Kagera Sugar wakasawazisha.

Meshack Abraham alianza kuipatia Kagera Sugar bao dakika ya kwanza, kabla ya Erick Mwijage kufunga la pili dakika ya 33.

Kipindi cha pili, Biashara United walikuja juu na kufunga mabao matatu, la mkwaju wa penalti dakika ya 51 likiwekwa vyavuni na Collins Opare ambaye baadaye alikosa tena penalti kwa kugongesha nguzo, Baron Okech alifunga la pili dakika ya 81, dakika mbili baadaye Ambroce Awio akaweka la tatu.

Dakika nne za nyongeza, faulo iliyopigwa na David Luhende ilikwenda moja kwa moja wavuni na kuwaokoa Kagera Sugar, ikiiweka mechi hiyo kwenye rekodi.

Mechi ambazo zilikuwa zinaongoza kwa mabao mengi kabla ya hiyo ya juzi, ni ya Desemba 23, mwaka jana, Azam ikiifunga Ruvu Shooting mabao 4-1, kesho yake Simba ikiiadhibu KMC mabao 4-1 na siku hiyo hiyo, Costal Union iliitwanga Mbeya City 3-2.

# Miamba Ligi Kuu Z'bar yapeta Kombe la FA

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

TIMU za Ligi Kuu Zanzibar zimepeta katika hatua ya awali ya michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka visiwani hapa (ZFF) maarufu kama FA Cup, iliyoanza kutimua vumbi juzi, Januari 15.

Hiyo ni baada ya kuibuka na ushindi juzi, ambapo Zimamoto ilishinda kwa mikwaju ya penalti 10-9 dhidi ya New Power ya Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja kutokana na dakika 90 kukamilika kwa kutoka suluhu kwenye mechi hiyo iliyopigwa katika Uwanja wa Mchangani.

Katika Uwanja wa Kinyasini, Maafande wa KVZ nao waliibuka na ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya timu ya Ujamaa ya Ligi Daraja la Pili Mkoa wa Kusini.

Lakini JKU ndio timu pekee kutoka Ligi Kuu kwa jana iliyoambulia kichapo cha bao 1-0 dhidi ya Ngome ya Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja mchezo ukipigwa katika Uwanja wa Ngome, Fuoni.

Akizungumza na gazeti hili Kocha Mkuu wa Timu ya Zimamoto, Mohmed Ali 'Kocha Tedy', alisema licha ya kupita hatua ya awali kwa mikwaju ya penalti, alikiri mchezo huo kuwa mgumu.

Alisema timu za madaraja ya chini zinapokutana na zile za Ligi Kuu, zinacheza rafu sana ili kupata ushindi wa kulazimisha ndio maana mchezo unakuwa mgumu kwa dakika zote.

Alisema Zimamoto ilicheza kwa tahadhari katika dakika zote kwa kuwa walijua wapinzani wao watakuja na mbinu ya mchezo wa nguvu sana jambo ambalo linaweza kusababisha wingi wa majeruhi kikosini.

Ratiba ya Michuano hiyo mzunguko huu wa awali itaendelea tena leo kwa kupigwa michezo mitatu ambapo timu ya Polisi watawavaa Sharp Boys kwenye Uwanja wa Kinyasini huku Mlandege wakivaana na New Boys katika dimba la Amaan na timu ya Baharia wakipepetana na Dulla Boys katika Uwanja wa Kichakanyuki.

Michuano hiyo ya Kombe la FA ambayo haina udhamini inachezwa kanda mbili; Unguja na Pemba na kwa mujibu wa kanuni mshindi wa Kanda ya Unguja atakutana na mshindi wa Kanda ya Pemba na kupata bingwa wa michuano hiyo ambayo ataiwakilisha Zanzibar katika michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika CAF msimu ujao.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ADA YA HAALAND YAANIKWA

REAL Madrid au Barcelona lazima zitumie euro milioni 350 kumsajili straika wa Norway, Erling Braut Haaland kutoka Borussia Dortmund kwa mujibu wa wakala wake, Mino Raiola. ***(Marca)***

### BENITEZ KUSEPA EVERTON

KOCHA wa Everton, Rafael Benitez amekubali kuachana na klabu hiyo, huku Duncan Ferguson akitajwa kuchukua nafasi yake. ***(90 Min)***

### PHILLIPS KUONDOKA LEEDS

KIUNGO wa Leeds United, Kalvin Phillips, 26, anatakiwa na Liverpool, lakini Leeds wapo tayari kumwachia mchezaji huyo, huku Paris St-Germain, Bayern Munich na Real Madrid zikihusishwa naye. ***(El Nacional)***

### DE JONG BEI JUU BARCA

CHELSEA lazima iongeze ofa ya ya pauni milioni 33 kama wanataka kumsajili nyota wa Barcelona, Frenkie de Jong, 24. Barca inataka pauni milioni 60 kumwachia mchezaji huyo raia wa Uholanzi. ***(El Nacional)***

### POCHETTINO KUTUA MAN UTD

KOCHA wa Paris St-Germain, Mauricio Pochettino amehusishwa na mpango wa kutua Manchester United. ***(Telegraph)***

### ERIKSEN AGOMBEWA ULAYA

KIUNGO wa Denmark, Christian Eriksen, 29, ambaye alipatwa na shambulio la moyo kwenye michuano ya Euro 2020, anawaniwa na klabu kadhaa, huku akitarajia kukamilisha usajili wake wiki hii. ***(Times)***

### SALAH MSHAHARA MKUBWA

MSHAMBULIAJII wa Misri, Mohamed Salah, anataka mshahara wa pauni 400,000 kwa wiki ili asaini mkataba mpya Liverpool. Mkataba wa sasa wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, unamalizika kipindi cha majira ya joto mwaka 2023. ***(Mirror)***

### COSTA ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL imefanya mazungumzo na straika wa zamani wa Chelsea, Diego Costa, 33, huku akitarajia kuondoka Atletico Mineiro mwezi huu. ***(Goal)***

### CARLOS ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inatarajia kuendelea na mazungumzo na Sevilla wiki ijayo ili kumsajili nyota wa Brazil, Diego Carlos, 28. ***(90 Min)***


### FIRMINO AWANIWA BARCA

BARCELONA imeonyesha nia ya kutaka kumsajili, Roberto Firmino kutoka Liverpool ambaye ada yake ni euro milioni 20. ***(El Nacional)***

### RANGNICK AHOJI USAJILI UTD

KOCHA wa muda wa Manchester United, Ralf Rangnick amehoji kwa nini timu hiyo haisajili kipindi hiki cha dirisha dogo. ***(Mirror)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




# MARTIAL HAKUTAKA KUIVAA ASTON VILLA - RANGNICK

**MANCHESTER,** England

**Angekuwa kwenye kikosi kama kawaida, lakini yeye mwenyewe...**

ANTHONY Martial "hakutaka" kuwapo kwenye kikosi cha Manchester United kilichotoka sare ya mabao 2-2 na Aston Villa, amedai kocha wa 'Mashetani Wekundu' hao, Ralf Rangnick, wakati straika huyo akiendelea kulazimisha kuondoka Old Trafford.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 26, hakuwapo kwenye kikosi cha Rangnick ambaye alitaja wachezaji nane kwenye benchi wakati United ikielekea kule Villa Park, ambako Philippe Coutinho alifunga bao dakika za majeruhi ili kupata sare hiyo.

**Rangnick tayari alikuwa bila Marcus Rashford na Cristiano Ronaldo kutokana na majeraha, huku Anthony Elanga akichaguliwa kuanza winga ya kushoto.**

Kocha huyo wa muda wa United alibainisha mwezi uliopita kwamba, raia huyo wa Ufaransa, Martial anataka kuondoka kutoka klabuni hapo kutokana na kukosa dakika za kutosha za kucheza.

Sevilla iliripotiwa kuwania kumsajili Martial, lakini walishindwa kufikia mshahara wake, huku United ikikataa kumtoa kwa mkopo hadi mwishoni mwa msimu huu.

Martial alionekana kutokataa kucheza kwenye mchezo huo wa sare dhidi ya Aston Villa na Rangnick amebainisha wazi. Rangnick aliwaambia waandishi wa habari: "Hakutaka kuwapo kwenye kikosi.

"Angekuwa kwenye kikosi kama kawaida, lakini yeye mwenyewe hakutaka na ndio maana hakusafiri na sisi."


SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
MBEYA CITY
VERSUS
SIMBA
1 | 5.76
X | 3.12
2 | 1.65

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# DYBALA APONDA SOKA LA JUVENTUS



**TURIN,** Italia

PAULO Dybala amesema Juventus "haichezi soka zuri" baada ya kukataa kushangilia bao lake katika ushindi wa mabao 2-0 kwenye Serie A dhidi ya Udinese.

Majaliwa ya Dybala yapo shakani huku mkataba wa raia huyo wa Argentina ukiwa unafikia ukingoni mwishoni mwa msimu huu na nyota huyo mwenye umri wa miaka 28 akihusishwa na kuhamia Inter Milan.

Hakusherehekea bao lake la ushindi pale Allianz huku wachezaji wenzake wakimfuata kumpongeza.

Alipoulizwa kama hiyo ilikuwa ishara kwa wakurugenzi wa klabu hiyo kuhusu majadiliano ya mkataba mpya, Dybala aliiambia Sky Sport Italia: "Nilimwalika rafiki na hakuweza kuona. Kuna watu wengi walikuwa pale na sikuweza kumuona."

Baada ya kuulizwa kama alikuwa anazungumza ukweli, Dybala alijibu: "Sijui, hiyo ni shauri yako.

"Kumekuwa na habari nyingi, na vitu vingi vimetokea na mimi nimeamua kutokuzungumza sana."



## Tuchel amchana tena Lukaku

**LONDON,** England

THOMAS Tuchel hakufurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na Romelu Lukaku baada ya Chelsea kufungwa bao 1-0 na Manchester City pale kwenye Uwanja wa Etihad.

Bao kutoka kwa Kevin De Bruyne lilikifanya kikosi cha Pep Guardiola kuongoza kwa tofauti ya pointi 13 katika msimamo wa Ligi Kuu England dhidi ya Chelsea, huku 'Blues' hao wakishinda mechi nne tu kati ya 12 za ligi zilizopita.

Lukaku hakuwa kwenye kiwango bora katika mchezo huo, akigusa mpira mara 21 tu na hakupiga shuti lolote langoni.

Mchezaji huyo aliyesajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi ya pauni milioni 97 kutoka Inter, hivi karibuni aliomba radhi baada ya kutamka hadharani kuwa hana fura ha hapo Chelsea.

Akizungumza na BT Sport baada ya mchezo huo Tuchel alielezea kutoridhika kwake na kiwango cha rai huyo wa Ubelgiji, akisema "Alipoteza mipira mingi n hakuwa na presha yoyote.

"Tunataka kumsaidia yeye ni sehemu ya timu na kwa hakika kabisa tu nategemea mengi kutok kwake.

## HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO
JISAJILI CHEZA SHINDA

# USAJILI KILI MARATHON WASHIKA KASI HUKU MUDA UKIYOYOMA

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI ukiwa umebaki mwezi mmoja na siku chache kabla ya mbio za Kilimanjaro Premium Lager Marathon kufanyika, usajili unaendelea kushika kasi huku waandaaji wakitoa wito kwa washiriki wajisajili mapema kuepusha usumbufu.

Taarifa iliyotolewa na waandaaji wa mbio hizo jijini Dar es Salaam jana, imeeleza punguzo la asilimia 20 lililokuwapo tangu Oktoba mwaka jana kwa ajili ya ada ya kujisajili, lilimalizika Januari 7, mwaka huu.

Tayari ada za mbio tofauti zimepanda isipokuwa kwa kilometa tano huku wakitoa wito kwa washiriki wajisajili mapema kuepusha usumbufu dakika za mwisho kwani mbio hizo zinaadhimisha miaka 20 tangu kuanzishwa kwake.

"Punguzo hili limekuwapo tangu Oktoba 17, mwaka jana wakati usajili ukifunguliwa rasmi na bei za usajili zimepanda sasa," ilisema taarifa hiyo na kuongeza kuwa usajili ni kwa njia ya mtandao www.kilimanjaromarathon.com au kwa njia ya Tigo Pesa kwa kubonyeza*149*20#.

Awali, Watanzania na wananchi wa Afrika Mashariki walikuwa wanalipa Sh. 25,000 kwa mbio za Km. 42 na 21 na za kilometa tano kwa Sh. 5,000 lakini sasa wameanza kulipa Sh. 30,000 kwa mbio za Km 42 na 21 na kilometa tano imebaki bei ile ile ya Sh. 5,000.

Kwa mujibu wa waandaaji hao, wakazi wa Tanzania na wa Afrika Mashariki wenye vibali vya kazi au vya ukaazi na wananchi wa SADC walikuwa wanalipa dola 40 kwa mbio za Km 42 na 21, lakini kuanzia Januari 8, mwaka huu, walianza kulipa dola 50 wakati kilometa tano imebaki kuwa dola tano.

"Washiriki wa kimataifa walikuwa wanalipa dola 80 ila kuanzia Januari 8, mwaka huu walianza kulipa dola 90 kwa Km. 42 na 21 na kilometa tano imebaki kuwa dola tano," ilieleza taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilisema usajili utafungwa saa sita usiku wa Februari 7, mwaka huu au pale ambapo nafasi zitajaa hata kama ni kabla ya tarehe hiyo.

"Tunatoa wito kwa washiriki wote wazingatie tarehe hizi kuepuka usumbufu kwani huenda namba zote zikaisha kama miaka ya nyuma huku ikizingatiwa kuwa mwaka huu tunaadhimisha miaka 20," ilieleza taarifa ya waandaaji wa mbio hizo.

Aidha, ilieleza mbio hizo, zilizoanza na washiriki wasiozidi 500 waliokimbia kwa kujifurahisha, sasa zinajivunia washiriki zaidi ya 12,000 kutoka mataifa zaidi ya 55 na watazamaji wanaokaribia idadi hiyo ya washiriki.

Mbio za mwaka huu zitafanyika Jumapili Februari 27, 2022 katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU).

Wadhamini wa mbio za mwaka huu ni Kilimanjaro Premium Lager-Km. 42, Tigo- Km. 21, Grand Malt - kilometa tano, wadhamini wa meza za maji ni Absa, Unilever, TPC Sugar, Simba Cement, Kilimanjaro Water na wasambazaji maalumu Garda-World Security, Keys Hotel, Kibo Palace Hotel na CMC Automobiles.

Mbio za Kilimanjaro Premium Lager Marathon huandaliwa na Kilimanjaro Marathon Company Limited na kuratibiwa kitaifa na Kampuni ya Executive Solutions Limited.

# *Simba wapania tatu za Mbeya City leo*

**Na Mwandishi Wetu**

KUELEKEA mechi yao ya leo Ligi ya Kuu Bara, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, amesema watavaa Mbeya City kwa tahadhari kubwa ili kuhakikisha wanaondoka na alama zote tatu.

Simba itashuka katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya leo kuvaana na Mbeya City, huo ukiwa mchezo wao wa kwanza kwenye ligi hiyo tangu kutoka kutwaa Kombe la Mapinduzi visiwani Zanzibar.

Akizungumza na Nipashe jana, Pablo alisema anafahamu utakuwa mchezo mgumu kutokana na ubora wa Mbeya City, lakini ukichagizwa na aina ya uwanja watakaotumia.

Kwa upande wa beki wa kulia wa timu hiyo, Shomari Kapombe, alisema wanaenda kuivaa Mbeya City ambayo ina michezo mizuri kwenye Ligi Kuu na kwamba mechi iliyopita wamewaona wanacheza vizuri na wapo imara, hivyo wamejiandaa kwa ajili ya kuwavaa.

"Tumetoka kufanya vizuri Kombe la Mapinduzi na kutwaa kombe, lakini tunakuja katika mchezo huu tukiwa waangalifu ili kufanya vizuri na kuanza mwaka vizuri na [hatimaye] kutetea ubingwa wetu," alisema Kapombe.

KAPATIA...




Mshindi wa Jackpot ya SportPesa, Enos Paul Nzagamba kutoka Geita, akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 10.2 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita. Jackpot inayoshindaniwa wiki hii imefika Sh. 846,297,200/-. **PICHA: SPORTPESA**

SPORTPESA APP
PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATATU - 17/01/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 2708 | Polisi Tanzania vs Namungo | 2.14 | 2.95 | 4.00 |
| 14:15 | 5723 | Bali Utd Pusam vs Persita Tangerang | 1.51 | 3.85 | 5.59 |
| 15:40 | 2808 | AL Khlood vs Hajer Club | 3.09 | 2.94 | 2.29 |
| 16:00 | 2099 | Gasogi United vs Gicumbi | 1.76 | 3.18 | 4.63 |
| 16:00 | 3926 | Mukura vs Police FC Rwanda | 2.75 | 3.04 | 2.46 |
| 16:00 | 4779 | Mbeya City vs Simba | 5.76 | 3.12 | 1.65 |
| 16:00 | 5035 | Crystal Palace U23 vs Chelsea U23 | 2.12 | 3.61 | 2.84 |
| 16:20 | 4288 | Al Arabi Doha SC vs Qatar SC | 2.93 | 3.27 | 2.21 |
| 16:45 | 3268 | Psis Semarang vs Arema | 4.52 | 3.36 | 1.72 |
| 17:00 | 4108 | Hyderabad FC vs Jamshedpur | 2.28 | 3.17 | 2.89 |
| 17:45 | 1423 | AL Nahdha vs Al Qadisiyah | 3.28 | 3.04 | 2.14 |
| 18:30 | 1118 | Al Ahli Doha SC vs AL Wakrah | 3.42 | 3.32 | 1.97 |
| 18:30 | 3866 | Al-Sailiya SC vs Lekhwiya SC | 16.43 | 8.70 | 1.08 |
| 19:00 | 3013 | Burkina Faso vs Ethiopia | 1.63 | 3.52 | 5.75 |
| 19:00 | 3654 | Cape Verde vs Cameroon | 5.14 | 3.41 | 1.72 |
| 19:30 | 2055 | AL Draih vs Jeddah Club | 2.84 | 3.03 | 2.39 |
| 20:00 | 1140 | Hapoel Afula vs Hapoel Ramat Gan | 2.44 | 3.08 | 2.98 |
| 20:00 | 1285 | AS Ashdod vs Beitar Tel Aviv Ramla | 1.53 | 3.91 | 6.14 |
| 20:00 | 1987 | El Fahem vs Ironi Hasharon | 2.40 | 3.16 | 2.96 |
| 20:00 | 3387 | Bnei Yehuda vs Maccabi Bney Reine | 1.75 | 3.42 | 4.86 |
| 20:00 | 3898 | Genclerbirligi vs Adanaspor | 1.28 | 5.00 | 8.46 |
| 20:00 | 5034 | SC Kfar Qasem vs Ahi Nazareth | 2.39 | 3.07 | 3.07 |
| 20:30 | 2957 | Bologna vs Napoli | 3.75 | 3.55 | 1.95 |
| 20:30 | 5158 | AC Milan vs Spezia | 1.29 | 5.60 | 9.40 |
| 21:00 | 1028 | Maccabi Netanya vs Bnei Sakhnin | 1.79 | 3.39 | 4.06 |
| 21:00 | 1040 | Waldhof Mannheim vs Borussia Dortmund II | 2.04 | 3.44 | 3.34 |
| 21:00 | 1164 | Sporting Farense vs Leixoes | 1.77 | 3.47 | 4.30 |
| 21:30 | 1676 | Club Nxt vs OH Leuven U21 | 1.22 | 5.96 | 8.84 |
| 21:30 | 1701 | Anderlecht U21 vs Cercle Brugge U21 | 1.28 | 5.59 | 7.13 |
| 21:30 | 1938 | Hapoel Beer Sheva vs Maccabi Haifa | 3.57 | 3.18 | 1.98 |
| 21:30 | 1993 | St Truiden U21 vs KRC Genk U21 | 3.50 | 3.93 | 1.78 |
| 21:30 | 2389 | Kortrijk U21 vs Mouscron U21 | 3.97 | 3.87 | 1.69 |
| 21:30 | 2421 | Zulte Waregem U21 vs Charleroi U21 | 2.79 | 3.75 | 2.11 |
| 21:30 | 4680 | KAA Gent U21 vs Mechelen U21 | 1.11 | 7.72 | 14.47 |
| 21:30 | 5116 | Antwerp U21 vs Standard Liege U21 | 4.24 | 4.24 | 1.59 |
| 22:00 | 2086 | Jong Ajax vs Den Bosch | 1.38 | 5.07 | 6.04 |
| 22:00 | 2107 | Tottenham U23 vs Blackburn Rovers U23 | 1.39 | 4.98 | 5.56 |
| 22:00 | 2552 | Wolverhampton U23 vs Burnley U23 | 1.92 | 3.61 | 3.32 |
| 22:00 | 2863 | Swansea U23 vs Bristol City U23 | 3.26 | 4.03 | 1.83 |
| 22:00 | 3600 | Lierse SK vs Waasland Beveren U21 | 3.10 | 3.85 | 2.09 |
| 22:00 | 4702 | Lommel U21 vs Excelsior Virton U21 | 3.03 | 3.95 | 1.93 |
| 22:00 | 5583 | Dordrecht vs Jong AZ Alkmaar | 2.97 | 3.46 | 2.17 |
| 22:00 | 5627 | West Bromwich U23 vs Aston Villa U23 | 2.36 | 3.72 | 2.46 |
| 22:45 | 1282 | Cliftonville Belfast vs Glentoran Belfast | 2.74 | 3.32 | 2.30 |
| 22:45 | 1582 | Celtic vs Hibernian | 1.31 | 5.10 | 8.44 |
| 22:45 | 3691 | Laval vs Annecy FC | 2.46 | 3.10 | 2.81 |
| 22:45 | 4160 | Chelmsford vs St.Albans | 2.80 | 3.38 | 2.23 |
| 22:45 | 4402 | Paris FC vs Le Havre | 2.03 | 3.09 | 3.78 |
| 22:45 | 5466 | Fiorentina vs Genoa | 1.41 | 4.70 | 7.21 |
| 23:15 | 3344 | Portimonense vs Vitoria Guimaraes | 2.57 | 3.16 | 2.71 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Januari 17, 2022

Nipashe




Tuchel amchana tena Lukaku

UKURASA 22

USHINDI NA USHINDI!...




Usajili mpya wa Yanga mshambuliaji kutoka TP Mazembe, Chico Ushindi na Kocha wa zamani wa Makipa wa Simba, Mbrazil Milton Nienov, ambao wametambulishwa jana kabla ya mechi dhidi ya Coastal Union katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, mchezo uliomalizika kwa Yanga kuibuka na ushindi wa mabao 2-0. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Yanga yavunja rekodi kibabe Mkwakwani*

## Ni wakati ikimtambulisha Ushindi na kocha Mbrazil wa…

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya misimu sita ya kutopata ushindi wowote dhidi ya Coastal Union kwenye Uwanja wa Mkwakwani Tanga, hatimaye jana Yanga ilizima mzimu huo mbaya, ilipoichakaza timu hiyo mabao 2-0 kwenye mechi ya raundi ya 12 ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Mara ya mwisho kwa Yanga kushinda uwanjani hapo ilikuwa Februari 4, 2015 ikiwa ni mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2014/15 kwa bao 1-0 lililowekwa wavuni na aliyekuwa nahodha wa timu hiyo wakati huo, Nadir Haroub 'Cannavaro' dakika ya 11 tu ya mchezo.**

Kwa misimu yote hiyo, Yanga imecheza mechi tano kwenye Uwanja wa Mkwakwani, ikipoteza mechi mbili na kutoka sare tatu.

Msimu uliopita, Machi 4, mwaka jana, Yanga ilipoteza mechi dhidi ya Coastal Union kwa mabao 2-1 kwenye uwanja huo. Lakini jana yalikuwa ni mabao ya wachezaji wawili wa kimataifa, Mkongomani Fiston Mayele na Mrundi Saido Ntibazonkiza yaliyomaliza rekodi mbaya ya Yanga, Uwanja wa Mkwakwani, Tanga.

Mayele alianza kwa kuikosesha timu yake bao dakika ya tano ya mchezo, baada ya kupewa pasi ya zawadi kutoka kwa beki wa kushoto wa Coastal Union, Mbaraka Hamza aliyerudisha nyuma mpira bila kuangalia na kumkuta straika huyo hatari ambaye shuti lake lilitoka nje, huku kila mmoja akiamini mpira ungejaa wavuni.

Dakika moja tu baadaye, beki Hamza aliyetaka kusababisha timu yake kufungwa, alipanda mbele na kumegewa pande safi kutoka kwa Abdul Selemani 'Sopu', lakini shuti lake lililopaa juu.

Mayele, akiwa amekabwa na mabeki wa Coastal Union, aligeuka ghafla na kupiga shuti la mguu wa kushoto lililotoka sentimeta chache nje ya lango, dakika ya nane tu ya mchezo.

Saido Nibazonkiza dakika ya 11, aliupata mpira pembeni mwa uwanja na kuukokota kwa muda mrefu, akiingia ndani ya eneo la hatari la wenyeji wao, badala ya kutoa pasi rahisi kwa wenzake waliokuwa wamejipanga vema, aliamua kupiga shuti lililokwenda juu la lango.

Baada ya kosa kosa hizo, mpira ulionekana kuchezwa kati zaidi, ndipo dakika tano kabla ya mapumziko, Mayele aliporekebisha makosa yake kwa kupachika bao la kwanza.

Ulianza mpira wa faulo langoni mwa Coastal Union ambao ulikuwa unaokolewa kizembe na kushusha kizaazaa, ukapigwa upande wa kulia kwa Djuma Shaaban ambaye alipiga krosi 'dongo' iliyomkuta mfungaji akiwa peke yake, akafunga kirahisi.

Kipindi cha pili Coastal Union waliingia kwenye mtego wa Yanga kupoozesha mpira na kupiga mipira ya juu.

Kipa Abdultwalib Mshery aliokoa mpira uliopigwa kichwa na Victor Patrick, akaruka juu na kuupangua, kabla ya kugonga mwamba wa juu na kutoka nje, ikazaa kona ambayo haikuwa na madhara.

Shambulio la kushtukiza dakika moja kabla mechi kumalizika, liliipatia bao la pili, baada ya mabeki watatu kutegeana kuokoa mpira na kunyang'anya mpira na Farid Mussa, aliyekuwa ndani ya eneo la hatari, akaurudisha nyuma na kumkuta Ntibazonkiza ambaye alipiga shuti ambalo kipa Mbissa hakujaribu hata kujishughulisha.

Ni matokeo yanayoendelea kuiweka salama Yanga kileleni ikiwa imefikisha pointi 32 kwa mechi 12, huku Coastal ikibaki nafasi ya tatu kabla ya mechi za leo, ikiwa na pointi 17.

Wakati huo huo klabu ya Yanga imewatambulisha uwanjani hapo na kwenye mtandao wake wa instagram, mchezaji Chico Ushindi kutoka TP Mazembe na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, pamoja na aliyekuwa kocha wa makipa wa zamani wa Simba, Milton Nienov.

Chico anachukua nafasi ya Mukoko Tonombe ambaye amejiunga na miamba hiyo ya Congo DR, na Milton ambaye huenda akachukua nafasi ya Razack Siwa.

# Pablo atoa sababu kumkubali Chama

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Pablo Franco, amesema kuzungumzwa kwa hali isiyo ya kawaida na mashabiki wengi wa soka nchini, kulimfanya kulazimika kuanza kuziangalia video za mchezaji Clatous Chama ambaye amerejea tena kwenye klabu hiyo akitokea RS Berkane ya Morocco.

Akizungumzia ujio wa mchezaji huyo, kocha huyo raia wa Hispania, alisema yeye ndiye aliyeamua mchezaji huyo arejee nchini kama uwezekano huo upo, baada ya kupitia video zake mbalimbali.

"Angekuwa mchezaji wa kawaida asingekuwa anazungumzwa kiasi kile, kila unapopita na kila kukicha, jambo lililinifanya hata mimi nianze kumfuatilia sana ili kuuona uwezo wake. Nikaziangalia video zake mbalimbali, nikakubaliana na uwezo wake, ndiyo maana sikutaka kuweka kikwazo katika urejeo wake, tukakubaliana wote arudi," alisema kocha huyo.

Alisema kuwa Chama ni mchezaji mzuri sana na anaamini ataisaidia timu kwa kushirikiana na wenzake kwa sababu ana uwezo mkubwa na ana imani naye.

Kauli hiyo ya Pablo imefuta dhana kuwa viongozi wa Simba wamemrudisha mchezaji huyo bila kumshirikisha.

Urejeo wa Chama, raia wa Zambia umeonekana kuwa ni ahueni kwa wanachama, wapenzi na mashabiki wa Simba ambao walikuwa wakimwimba kila kukicha.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >